epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Mei 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581671
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**MAN UNITED HAINA HARAKA NA TEN HAG**

# Vyama vyaonyesha shaka uchaguzi huru na wa haki

• **Vyadai** kanuni hakuna, daftari la wapigakura limechezewa...*Endelea ukurasa 2*



"Kuna dalili za kutosha uchaguzi serikali za mitaa ukasimamiwa na TAMISEMI, jambo linalopingwa vikali na vyama vya upinzani.

**Prof. Ibrahim Lipumba**



"Tunakwenda kwenye uchaguzi hatujui kanuni zitatoka lini, wanaficha kila kitu, hata ukiangalia mabadiliko ya sheria za uchaguzi hayawezi kutibu matatizo yaliyokuwapo.–

**Freeman Mbowe**



"Wapinzani waache kuendeleza hofu kwa kuwa wanaweza kufa hata kabla ya wakati.

**Dk. Mohamed Dimwa**

# Bunge laagiza uchunguzi wanafunzi wanaotumia dawa za kulevya shuleni



UKURASA 2

UKURASA WA 3

## MAAGIZO SABA YA RAIS SAMIA NISHATI SAFI



RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo saba kuhusu nishati safi ikiwamo Wizara ya Nishati kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa...

UKURASA WA 5

## ACT WAZALENDO YATOA NENO KUHUSU BAJETI FINYU ELIMU



CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kuna haja serikali kutenga bajeti ya Sh.bilioni 50.2 ili kuongeza idadi ya ajira za walimu kwa shule za msingi, sekondari na...

UKURASA WA 4

## WHO, TAASISI 11 KUIMARISHA AFYA KWA UMMA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetiliana saini makubaliano na taasisi 11 yakiwamo mashirika...

## Ongezeko maji Ziwa Victoria laacha maafa

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA, AZAM FC VITA YA NAFASI YA PILI UK.24

**KATUNI** UK.6

# Vyama vyaonyesha hofu uchaguzi huru na haki

**Na Halfani Chusi**

VIONGOZI wa vyama vya siasa wameeleza hofu kuhusu uwezekano wa Tume Huru ya Uchaguzi kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu wa mwakani.

Wamesema hofu hiyo inatokana na daftari la kudumu la wapigakura na kanuni za uchaguzi kutowekwa hadharani.

Viongozi hao walionyesha hofu hiyo jana katika mkutano wa kitaifa kutafakari na kujenga uelewa wa pamoja kuhusu sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba, mwaka huu na uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, 2025.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, ambaye ni Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) walionyesha hofu hiyo huku Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said, akiwataka waache hofu kwa kuwa wanaweza kufa kabla ya wakati.

Profesa Lipumba alisema pamoja na mabadiliko ya sheria hiyo, anaona kuna dalili za kutosha uchaguzi ukasimamiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), huku akisisitiza kuwa ni jambo linalopingwa vikali na vyama vya upinzani. Alishauri kwamba hawapaswi kuwapuuza kwa kuwa lengo ni kujenga demokrasia ya nchi.

"Demokrasia si jambo la magharibi, si jambo la mashariki bali ni jambo la ulimwengu mzima. Mwalimu (Julius) Nyerere alikuwa akisisitiza kwamba hata kwenye vijiji vya kiasili, palikuwa na demokrasia watu wanafanya uamuzi chini ya mti.

"Sheria ambayo imepitishwa inasema jukumu la Tume Huru ya Uchaguzi ni kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa. Sasa hili likoje kwamba sheria tayari imepitishwa lakini itasimamiwa na TAMISEMI? Labda pana maelezo ya namna gani katika kipindi hiki cha mpito," alisema.

Akichangia mjadala huo, Mbowe alisema kinachokwamisha matakwa ya vyama vya upinzani kuhusu sheria za uchaguzi ni kile alichodai CCM ina maslahi binafsi katika hilo.

"CCM wana manufaa na sheria za uchaguzi. Yako mengi yanafanyika kwa makusudi tutaweza kulaumu uchaguzi uliopita kwa yaliyofanyika lakini ukweli utabaki kuwa ukweli.

"Daftari la Kudumu la Wapigakura lililopo leo lilichezewa sana mwaka 2020. Ni jambo la kujiuliza tutakwenda kuliboresha au kuandikisha upya? Tuna tatizo la kuangalia mbele bila kuangalia tulijikwaa wapi. Huwezi kufanya mabadiliko bila kuanzia kwenye katiba.

"Tunakwenda kwenye uchaguzi hatujui kanuni zitatoka lini. Wanaficha kila kitu. Hata ukiangalia mabadiliko ya sheria za uchaguzi hayawezi kutibu matatizo yaliyokuwapo na haiakisi haki katika uchaguzi ujao," alisema.

Alisema katika vikao vya maridhiano walivyokaa mwaka mzima, walijadili masuala ya uchaguzi kwa kina na hata TCD, kikosi kazi, asasi za kiraia na taasisi za dini pia walijadili lakini kwasababu kuna kiburi, CCM hawayataki mambo hayo.

"Hata tungefanya maboresho ya sheria kiasi gani kama upande wa pili hakuna utashi wa kisiasa, hivyo tutakuwa tunapoteza muda. Yale tuliyokuwa tunalalamikia mwaka 2019 na 2020 mpaka leo 2024 yanaendelea kufanyika licha ya wadau wote kuishauri serikali ya CCM ambayo imekuwa haisikii. Yenyewe inapenda kufanya yale ambayo inakuwa faida kwao," alisema.



Magari na pikipiki yakipita kwa shida kwenye barabara mbovu inayohitaji ukarabati ya Mwenge Madukani, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara na wateja wanaofika katika eneo hilo. **PICHA: JOHN BADI**

## BRELA yaja kampeni elimu miliki bunifu

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeanzisha kampeni maalum ya kutoa elimu kwa wadau wote muhimu wa miliki bunifu nchini kwa kutoa elimu kwenye makundi mbalimbali vikiwamo vyuo vikuu na vyuo vya ufundi stadi nchini.

Mkurugenzi wa Miliki Bunifu wa BRELA, Loy Mhando, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya miliki bunifu yanayofanyika leo jijini Dar es Salaam.

Maadhimisho hayo yanatarajiwa kufunguliwa leo na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, na kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Miliki Ubunifu na Malengo ya Maendeleo Endelevu: Kujenga Mustakabali wa Pamoja kwa Kutumia Ubunifu'.

Alisema BRELA imeamua kuja na kampeni hiyo baada ya kubaini kuwa wananchi wengi hawafahamu vyema kuhusu miliki bunifu hivyo wamepanga kuwafikia watu wengi ili waweze kuwa na ufahamu kuhusu miliki bunifu.

"Tumekwenda vyuo vikuu, tumeongea na wawekezaji na wajasiriamali na tunaushirikiano na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ili kuwafikia wabunifu wa teknolojia za aina mbalimbali kwasababu tume hiyo inaangalia teknolojia na ubunifu," alisema.

Alisema kupitia ushirikiano huo wameshatambua teknolojia zilizovumbuliwa na vijana kwenye mikoa mbalimbali ambako wametambua teknolojia za vijana 25 na BRELA imewashauri waziweke kwenye namna ambayo italeta suluhisho la matatizo mbalimbali ya kijamii.

"Lakini tunahakikisha bunifu zao zinapatiwa ulinzi na kuzuia watu wengine kuzitumia bila ridhaa yao na hali hii inampa moyo mbunifu aendelee kubuni vitu vingine zaidi kwasababu anajua kazi zake zitalindwa na wakala," alisema.

# Bunge laagiza uchunguzi wanafunzi dawa za kulevya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeagiza serikali kufuatilia madai ya nusu ya wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Ukombozi iliyoko Kata ya Saranga, Ubungo mkoani Dar es Salaam kulala darasani asubuhi kwa kile kilichoelezwa kuwa ni matumizi ya dawa za kulevya.

Mwenyekiti wa Bunge, Deodatus Mwanyika, alitoa maelekezo hayo kwa serikali bungeni jana baada ya Mbunge wa Kibamba (CCM), Issa Mtemvu, kutoa taarifa hiyo kuwa kuna tatizo la maadili ya watoto ndani ya jimbo hilo.

"Katika Jimbo la Kibamba ambako Rais amejenga shule nzuri kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 400, Shule ya Ukombozi yenye watoto 1,400 ikifika saa 5:00 asubuhi, zaidi ya asilimia 70, yaani watoto 600, wameshalewa dawa za kulevya wanalala darasani. Hali hii ni mbaya kwa jamii," alisema Mtemvu alipokuwa akimpa taarifa mchangiaji ambaye ni Mbunge wa Tunduru Kaskazini (CCM), Hassan Kungu.

Kungu alisema anakubaliana na taarifa hiyo kwa kuwa ndio uhalisia na kwamba shule za sekondari bila kuwa na bweni wanafunzi wengi watapotea kimaadili.

Akizungumza wakati wa kuahirisha kikao cha bunge, Mwanyika alisema: "Kuna taarifa imetolewa na Mbunge wa Kibamba inaweza kuleta taharuki katika mazingira ambayo tunaongelea maadili. Tunaambiwa watoto saa tano mamia kwa mamia wamelewa, nadhani serikali mlifuatilie na kuleta taarifa ndani ya Bunge."

Baada ya maelekezo hayo, Mwanyika alimpa nafasi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, ambaye alisema amepokea maelekezo hayo na kwamba suala hilo limeishtua serikali kama shule ina zaidi ya watoto 1,000 na inapofika muda huo watoto 600 wanalala darasani kwa kulewa.

"Taarifa kidogo imetushtua kama serikali, tunapokea maelekezo yako kwa sababu tunafahamu serikali imejizatiti kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na nguvu ya pekee imewekwa kwa watoto wa shule za msingi na sekondari," alisema.

Alisema kwa mifumo ya elimu iliyopo kama kuna upungufu huo wa kushindwa kubaini suala hilo mapema itakuwa ni bahati mbaya.

"Kwa niaba ya serikali napokea maelekezo ya kiti na tutafuatilia ili kuwaokoa watoto na janga hilo na tufuatilie mifumo yetu inayoshindwa kujisimamia ili watoto kuenenda kwenye maadili mema," alisema.

## Serikali yaja na mwarobaini maslahi wazabuni wazawa

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema inafanya maboresho ya kanuni za ununuzi, ili kuhakikisha wazabuni wazawa wanalipwa fedha kwa wakati na kwa kiwango stahiki ambacho serikali ilikubaliana na mzabuni wa nje wakati wanaingia mkataba.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave, aliyetaka kufahamu kama serikali iko tayari kutoa maelekezo ili wafanyabiashara wa ndani kulipwa fidia pale malipo yao yanapocheleweshwa wa wawekezaji wa nje.

Swali hilo limeulizwa baada ya kuwapo malalamiko kutoka kwa wazabauni wazawa kucheleweshewa malipo yao na kulipwa kwa shilingi ya Tanzania ilhali mzabuni aliyeingia mkataba na serikali analipwa kwa Dola ya Kimarekani.

Dk. Nchemba alisema serikali inakamilisha mchakato kwa kurekebisha kanuni za manunuzi baada ya bunge kurekebisha Sheria ya Ununuzi wa Umma, lengo ni kuwaepusha na wazabuni wa ndani na ufumbufu kutoka kwa wazabuni wa nje ili na wao wanufaike na kazi wanazofanya.

Alisema ulipaji wa madai yanayotokana na kupokelewa kwa bidhaa au huduma huzingatia masharti ya mikataba ya zabuni au kandarasi iliyoingiwa baina ya serikali na mtoa huduma na serikali hulipa au hulipwa riba pindi masharti ya mikataba ya zabuni au kandarasi yanapokiukwa.

# Maagizo saba Rais nishati safi

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo saba kuhusu nishati safi ikiwamo Wizara ya Nishati kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa wadau wa sekta binafsi kufika vijijini na kuweka vituo vya kujazia gesi.

Amesema kuna Watanzania wengi wanapatiwa mitungi ya gesi, lakini baada ya kutumia na kuisha hawana mahali pa kujazia.

Rais Samia pia amemtaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, kuandaa katazo kwa taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100, kuwa ni marufuku kutumia kuni kupikia.

Alisema matumizi ya nishati safi ya kupikia ni mahitaji ya lazima na siyo hanasa.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa mkakati wa taifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ya 2024 -2034, Rais Samia alitaka Wizara ya Nishati, kufikisha mkakati huo kwa njia rasmi, kwa wadau wote muhimu, pamoja na kutafsiriwa kwa lugha mbili Kiswahili na Kingereza, ili wananchi wote waweze kuutumia.

"Pia wizara ikae na wadau husika serikalini ikiwamo sekta ya fedha na mipango na binafsi kubaini maeneo ambayo yakifanyiwa kazi yataongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa gharama himilivu, pamoja na kushirikiana na wadau muhimu kuhakikisha kunakuwa na mfuko wa kuendeleza nishati safi ya kupikia ifikapo 2025.

"Kwa pamoja tutajua jinsi ya kutafuta fedha zitakazoingia kwenye mfuko, pia tuone namna nishati safi ya kupikia itakavyoweza kutokea kwenye dira ya taifa ya mwaka 2050.

Pia alibainisha kuwa watathmini athari za kimazingira, kiuchumi na kiafya ni wazi kwamba, ukosefu wa nishati safi ya kupikia inarudisha nyuma jitihada za maendeleo ya nchi.

Alisema safari hiyo haiwezi kuwa kubwa ikiwa asilimia 90 ya wananchi bado wanatumia nishati isiyo rafiki. Rais Samia alisema serikali inajukumu la kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu nishati safi ya kupikia na kutunga sera nzuri wezeshi ili kufikia malengo ya mkakati huo.

"Katika hili Wizara ya Nishati watatuongoza kuhakikisha nishati safi ya kupikia inapatikana kwa uhakika na kwa bei inayohimilika kwa wananchi. "Sekta binafsi tunaitarajia pamoja na kuongeza uwekezaji, na upatikanaji wa nishati safi sehemu mbalimbali nchini, watuletee pia teknolojia itakayowezesha wananchi kupata nishati hiyo kadri ya uwezo wao.

Rais Samia alisema ni lazima wakuze na kuvutia uwekezaji zaidi katika uzalishaji wa majiko banifu, umeme na kuhamasisha uzalishaji wa vifaa vya gesi asilia nchini, akibainisha kuwa hatua hizo zitasaidia kupunguza gharama za nishati.

Aidha, alisema kuna haja serikali na sekta binafsi kukutana ili kuangalia namna ya kuongeza ubunifu katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazochangia matumizi madogo ya nishati safi, pamoja na kuangalia nani aliyeweza kuendelea kuongeza matumizi ya umeme kwa ajili ya kupikia.

"Lazima watu wabadilike, akiona mtungi wa gesi anasema ugali nitausongaje, maharage nitayapikaje, ubwabwa matandu nitayapatia wapi, lakini ladha ya chakula nikipikia kuni na hii ni tofauti.





Vigezo na Masharti Kuzingatiwa

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akifafanua jambo kwa Mkurugenzi wa Matengenezo kutoka Wakala wa Barabara (TANROADS), Dk. Christina Kayoza na Meneja wa TANROADS Mkoa wa Pwani, Mhandisi Baraka Mwambage, wakati akikagua urejeshaji wa miundombinu ya barabara kuu ya Lindi – Dar es Salaam eneo la Somanga mkoani Lindi jana. **PICHA: UJENZI**

# Ongezeko maji Ziwa Victoria laacha maafa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ONGEZEKO la kina cha maji katika Ziwa Victoria limesababisha athari katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Kanda ya Ziwa, ikiwamo ukosefu wa makazi kwa takriban kaya 519.

Kutokana na athari hizo, kumekuwa na hofu ya kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko pamoja na wanyama wakali kutoka ziwani.

Maeneo ambayo yameathirika zaidi kwa sasa ni Mwanza, Simiyu na Musoma ambako wastani wa usawa wa kina cha maji umeongezeka kutoka mita za ujazo 1,134 kutoka usawa wa bahari kwa mwaka 2023 hadi 1,134.86 kwa mujibu wa kipimo kilichofanyika Aprili 24, mwaka huu.

Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Gerald Itimbula, alitaja ongezeko hilo kuwa kubwa zaidi kutokea katika kipindi cha zaidi ya miaka 50.

"Wastani wa mvua iliyopimwa katika vituo 70 vya hali ya mvua kwa kipindi cha miezi ya Januari hadi Machi, mwaka huu ni milimita 124.2 tofauti na wastani wa muda mrefu katika kipindi hiki ambao huwa milimita 103.03," alisema Itimbula.

Pia alisema kwa mwezi Januari, walipata wastani wa mvua ya milimita 141 ambayo ni kubwa kulinganisha na wastani wa muda mrefu wa milimita 90.3, huku wastani wa mtiririko wa maji kutoka Mto Kagera ukitajwa kuongezeka kutoka mita za ujazo 198.28 kwa sekunde hadi 325.19 mwaka huu.

**ATHARI MIKOANI**

Ongezeko hilo la maji limesababisha athari mbalimbali katika mikoa ya Mwanza, Simiyu na Mara ambako yamesababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara pamoja na nyumba kuvamiwa na maji.

Katika mkoa wa Simiyu, kaya 413 katika vitongoji vya Lamadi, Makanisani na Itongo Kijiji cha Lamadi wilayani Busega, zimekosa makazi baada ya nyumba kuzingirwa na maji.

"Ni zaidi ya mita 600 kutoka katika eneo hili kuelekea ziwani lakini maji yamefika kwenye makazi na athari ni kubwa zikiwamo kuhama, magonjwa ya miguu na madhara hayo yameanza Aprili 28, mwaka huu," alisema Athuman Said.

Mkuu wa Wilaya ya Busega, Faidha Salim, alisema miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutenga maeneo ambayo waathirika watahamia ambayo ni shule ikiwamo Shule ya Sekondari Anthony Mtaka.

Mkoani Mwanza, ongezeko hilo limesababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara zilizoko kando ya ziwa, sehemu za kupumzika likiwamo eneo la Jiwe la Kihistoria la Bismark na kuvamia makazi ya watu.

"Sasa hivi hatuna pa kuishi maji yamejaa lakini inabidi tuishi humohumo kwenye maji licha ya kuwa kuna wanyama wakali wanaingia ndani wakiwamo nyoka pamoja na wadudu wengine ambao tunakabiliana nao hivyo hivyo," alisema Halima Haruna, Mkazi wa Mtaa wa Ziwa Victoria, Mwanza.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Abeid Mussa, alisema nyumba takriban 34 zimevamiwa na maji huku zaidi ya wananchi 80 wakiwa wamehama makazi yao huku wengine wakiendelea kubaki kwenye makazi hayo kutokana na kukosa mahala pa kuhamia.

"Tuna wasiwasi wa kuibuka kwa magonjwa kwani vyoo vimejaa na hapa maji tunayokanyaga ni hayo hayo bila kinga yoyote, hivyo tuko hatarini kwa sasa," alisema Grace Jumanne.

Wilayani Musoma mkoani Mara, pia hali hiyo imesababisha athari mbalimbali katika eneo la Kitaji ambako wakazi wa eneo hilo wanataja maji kujaa hadi kufunika vitanda hali inayosababisha watafute hifadhi katika maeneo jirani.

"Mimi ni mjane sina pa kwenda nalala hivyohivyo kwenye maji wala sina mtu wa kunisaidia kuondokana na hili naomba tu msaada wa serikali hata kwa kutafutiwa maeneo mengine salama," alisema Ashura Ally, mkazi wa Kitaji.

**KISIWA CHAZAMA**

Wilayani Musoma moja ya kisiwa cha Nyasahungu ndani ya Ziwa Victoria, kimetajwa kuzama kutokana na ongezeko hilo la maji. Kuzama kwa kisiwa hicho, kumesababisha makazi na zaidi ya kaya 20 kuzama ndani ya ziwa.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Halfan Haule, kutokana na kuzama kwa kisiwa hicho, serikali imechukua hatua ikiwamo kuwahamisha wananchi na kuwa hakuna vifo wala majeruhi.

Alisema shughuli kuu za wananchi katika kisiwa hicho ni uvuvi, hivyo wamepelekwa katika kisiwa kingine cha Kagongo na wanaendelea na shughuli zao.

Dk. Haule alisema licha ya kisiwa hicho kuzama, kingine cha Rubuka ambacho ni miongoni vya visiwa 12 katika wilaya hiyo, kaya nne zimeathirika.

Alisema kaya hizo kwa sasa zimehifadhiwa katika kituo cha Afya cha Rubuka huku zingine zikipata hifadhi kwa majirani na tayari kijiji kimekubali kuwapatia ardhi na tayari wameanza ujenzi wa nyumba za kudumu.

Wilayani Chato mkoani Geita ongezeko hilo limesababisha makazi na miundombinu kuvamiwa na maji ikimwamo ofisi ya kikundi cha usimamizi wa raslimali za uvuvi ndani ya Ziwa Victoria (BMU) katika mwalo wa Chato Beach.

# WHO, taasisi 11 kuimarisha afya kwa umma

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetiliana saini makubaliano na taasisi 11 yakiwamo mashirika yasiyo ya kiserikali na vyuo vikuu, kuimarisha mifumo ya afya kwa umma, kutoa elimu, kinga dhidi ya magonjwa na kufanya utafiti.

Miongoni mwa vyuo hivyo ni Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania, Rachel Chagonja, alitia saini pamoja na WHO kwa niaba ya taasisi hizo.

Chagonja alisema kwamba makubaliano hayo na WHO, yanabainisha nia ya dhati katika kuongeza wigo wa huduma za afya nchini na kuwafikia Watanzania.

Aiisema makubaliano hayo ambayo yana malengo yanayowiana na ya shirika hilo kwenye sekta ya afya, kwa kuwajengea uwezo wataalamu wa afya, kufanya utafiti na kuimarisha huduma za afya ngaji ya jamii.

"Tunaishukuru WHO kwa kushirikiana nasi kwenye sekta ya afya Tanzania. Tuitumie fursa hii kwa kufanya kazi pamoja, tukijenga afya na Tanzania itarajiwayo kwa Watanzania," alisema Chagonja.

Kuhusu manufaa ya makubaliano hayo, Mkuu wa DUCE, Prof. Stephen Maluka, alisema shirika hilo litasaidia wadau wa afya kutekeleza vipaumbele vya afya.

"Makubaliano haya yatasaidia ambao tunatoa elimu na wadau wa afya, kuboresha elimu ya lishe, afya ya uzazi, mama na mtoto pamoja na kinga. Ushirikiano huu, utasaidia kutekeleza vipaumbele vya serikali," alisema Prof. Maluka.

Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Apolinary Kamuhabwa, alisema mchakato wa kupatikana taasisi na mashirika 11 ulikuwa wenye ushindani, hivyo walioshinda fursa hiyo watafanya kazi bega kwa bega na WHO, ikiwamo kuandaa miongozo.

Mwakilishi Mkazi wa WHO Tanzania, Dk. Charles Sagoe-Moses, alisema makubaliano hayo yanatambua mchango mkubwa unaofanywa na mashirika na taasisi mbalimbali nchini, kwenye sekta ya afya, kuhakikisha hakuna anayeachwa kando katika afya.

"WHO inatambua thamani na kinachofanywa na taasisi hizi, kuboresha huduma za afya, hususan kwenye ajenda ya Afya Kwa Wote," alisema.

Alisema makubaliano hayo yatajikita katika kuimarisha mifumo ya afya, kinga dhidi ya magonjwa na Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs), magonjwa ya mlipuko na mtindo bora maisha.

## HABARI KITAIFA



Mwalimu Hellena Mabula ambaye ni mmoja wa walimu wanaofanya kazi na Taasisi ya SILABU APP inayotoa huduma za masomo ya ziada kwa wanafunzi majumbani na kwa njia ya mtandao, akichangia mada wakati wa semina ya mafunzo ya uelewa iliyotolewa na Benki ya NBC, baada ya taasisi hiyo kuingia makubaliano na benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi ya kusambaza elimu ya fedha kwa wanafunzi majumbani. **PICHA: JOHN BADI**

# ACT yatoa neno bajeti finyu elimu

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kuna haja serikali kutenga bajeti ya Sh.bilioni 50.2 ili kuongeza idadi ya ajira za walimu kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, kuongeza wakufunzi na wahadhiri angalau 5,000 ili kupunguza uhaba wa walimu vyuoni na vyuo vikuu.

Aidha, kimesema serikali itenge bajeti ya kutosha na kuongeza kiwango cha ruzuku kwa shule za msingi na sekondari kwa kiwango cha Sh. 25,000 kwa mwanafunzi wa shule ya msingi na Sh. 58,000 kwa mwanafunzi wa sekondari pamoja na kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera ya elimu kwa ajili ya ukaguzi na uthibiti ubora wa shule.

Kadhalika, chama hicho kimeiomba serikali kubeba gharama za ada, malipo ya mafunzo kwa vitendo, fedha za vitabu na viandikwa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na kwamba kufanya hivyo kutaondoa minyukano na kutatoa fursa sawa ya kupata elimu kwa wanafunzi bila kujali vipato vyao.

Waziri Kivuli wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wa ACT-Wazalendo, Hamidu Bobali, alisema hayo jana Dar es Salaam alipotoa taarifa ya tathmini ya uchambuzi wa bajeti ya Wizara hiyo ya mwaka wa fedha 2024/25 iliyowasilishwa juzi Bungeni Dodoma na Waziri mwenye dhamana.

Bobali alisema kufanya hivyo kutasaidia kuondoa matabaka ya watoto wa wenye nacho na wasio nacho kwenye kuwania elimu.

"Kwenye ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ACT-Wazalendo tulibainisha kuwa itafuta mikopo yote ya miaka ya nyuma iliyotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Italipa ada ya masomo, fedha za vitabu na gharama za mafunzo kwa vitendo kwa kila mwanafunzi anayedahiliwa kwenye chuo kikuu," alisema Bobali.

"Hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 haijajibu changamoto za muda wote kuhusu mfumo wa ugharamiaji wa elimu ya juu."

Kilipendekeza kwamba ni vema usimamizi wa sekta ya elimu ukasimamiwa na wizara moja badala ya tatu kama ilivyo sasa.

"Kugawanywa katika wizara takribani zaidi ya tatu yaani, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (kwa baadhi ya masuala) kuna fanya mpango wa bajeti kwenye sekta ya elimu kuyumbishwa kwa vipaumbele vyake," alisema Bobali.

Bobali alisema pamoja na Sera ya Elimu ya mwaka 2014 na mitaala yake kufanyiwa marekebisho na kuanza utekelezaji wake, bado kuna mambo yanahitaji marekebisho ambayo yatasaidia kuimarisha na kuboresha sekta ya elimu ikiwamo kuweka wazi lugha ya Kiswahili kuwa rasmi kufundishia na kujifunzia.

Alisema lugha hiyo inatakiwa kuwa ya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote na kupendekeza lugha nyingine zifundishwe kama somo.

Bobali alisema katika shule na vyuo, sera ya elimu haijaweka bayana juu ya lugha ya kufundishia kati ya Kiswahili na Kiingereza na hivyo, kuendeleza utata wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa ngazi ya awali na elimu msingi, huku katika ngazi ya sekondari na chuo ikitumika ya Kiingereza.

Jambo lingine ambalo alisema linahitaji marekebisho ni pamoja na suala la ugharimiaji wa elimu na mafunzo, kwamba sera hiyo haijaonyesha nani atagharamia upatikanji wa elimu katika kila ngazi, ijapokuwa imeonyesha wazi kuhusu uhaba wa bajeti na ongezeko na mahitaji.

# Mbaroni madai kunajisi mtoto, kumtoboa macho hatimaye kufa

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia mtu mmoja, mkazi wa Michese jijini hapa kwa tuhuma za kumnajisi na kumlawiti mtoto wa miaka miwili, hatimaye kumtoboa macho na kumsababishia kifo.

Aidha, jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa wawili kwa kosa la kukopesha watu kwa riba kubwa tofauti na ile iliyoelekezwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Theopista Mallya, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, alisema mtoto huyo aliokotwa ameshafariki dunia baada ya kupotea nyumbani kwa siku mbili.

"Mtoto huyu alipotea nyumbani kwa muda wa siku mbili na alikutwa akiwa ameshafariki dunia na mwili wake kutupwa eneo la jirani na nyumbani. Alipopimwa ilibainika kuwa alikuwa amenajisiwa na kulawitiwa pamoja na kutobolewa macho," alisema Kamanda Mallya.

"Mwili wa mtoto huyo unatarajiwa kuzikwa leo (jana) kwenye makaburi ya Michese jijini hapa," alisema.

Kamanda huyo alisema kutokana na tukio hilo, wanamshikilia mtu mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi huku wakiendelea na msako mkali kutafuta wahusika wengine kwa tukio hilo.

Alisema upelelezi bado unaendelea na mtuhumiwa yuko mahabusu kwa sababu za kiusalama, ikiwamo kulisaidia jeshi la polisi kupata taarifa sahihi za mauaji hayo ya kikatili.

Awali, akizungumzia tukio hilo alisema mtoto huyo alitoweka nyumbani siku mbili zilizopita na baadaye walimpata akiwa amefariki na kubainika kufanyiwa ukatili huo wa kutobolewa macho na kulawitiwa kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa daktari.

Kuhusu kuwashikilia wanaokopesha mikopo ya kausha damu, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Adrian Gervas kutoka Kampuni ya Microcredit na Said Ally kutoka kampuni ya Brown Finance.

Alisema watu hao wamekuwa wakikopesha watu kwa riba kubwa tofauti na ile ambayo BoT wameelekeza ilipwe kwenye mikopo.

Kamanda Mallya alisema watu hao wameachiwa kwa dhamana lakini watarejeshwa mahakamani kusomewa mashtaka yao pale upelelezi utakapokamilishwa na Jeshi la Polisi.

Pia alisema jeshi hilo limekamata mali mbalimbali zilizoibiwa kutoka maeneo mbalimbali ya jijini Dodoma. Mali hizo ni pamoja na runinga (Flat screen), pikipiki, friji, magodoro pamoja na vifaa mbalimbali.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utamaduni wa kuvumiliana muhimu kuelekea uchaguzi

**VIONGOZI** na wadau wa siasa, jana walikutana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa kitaifa kutafakari na kujenga uelewa wa pamoja kuhusu sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani uliopangwa kufanyika Oktoba, mwakani.

Katika mkutano huo uliowakutanisha viongozi wakuu wa vyama hivyo, kikiwamo chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) ziiibuliwa hoja mbalimbali ambazo zilionyesha dhahiri kwamba hamkani hali si shwari kuelekea kwenye mchakato huo. Hali hiyo ilionekana kutokana na baadhi ya viongozi wakuu wa vyama, hasa wa upinzani kuwa na madukuduku ambayo yanaweza kutia doa katika safari ya kwenda kwenye matukio hayo makubwa ya kidemokrasi ndani ya nchi.

Hofu kubwa zaidi imeonekana kwa viongozi hao kuonyesha wasiwasi wao kuhusu uwezo wa Tume Huru ya Uchaguzi katika kusimamia mchakato huo kama ambavyo sheria za uchaguzi ambazo zilipitishwa bungeni na hatimaye kutiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan zinavyobainisha.

Licha ya kuonyesha hofu ya uwezo wa tume, viongozi hao walibainisha kuwa uchaguzi huo huenda usiwe huru na haki kutokana na mazingira ya nyuma. Bila kuuma maneno wala kupepesa macho, walidai kuwa hali hiyo pia inatokana na daftari la kudumu la wapigakura lilichezewa katika uchaguzi uliopita na pia kanuni za uchaguzi hazijawekwa bayana.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF) na Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema haoni dalili za tume kwa mwaka huu na mwakani kuwa na uwezo wa kusimamia uchaguzi ulio huru na wa haki huku Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akigusia suala la daftari la kudumu la wapigakura ambalo alidai halijakaa vizuri kutokana na yale yaliyotokea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Pia aliweka bayana kwamba hata kanuni za uchaguzi hazijawekwa wazi. Kiongozi huyo hakuishia hapo bali alitupia lawama CCM kuwa ina maslahi na suala hilo na ndiyo inayoficha kanuni hizo na mchakato wa maboresho ya daktari la wapigakura. Wakati hofu hiyo ikitanda, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said, aliwapiga kijembe kuwa waache hofu kwa kuwa wanaweza kufa kabla ya wakati.


Siasa za kidemokrasia kama ulivyo mchezo wowote, zina ushindani, hivyo kinachotakiwa ni kuwa na kanuni na sheria zisizo na upendeleo wa upande wowote. Msimamizi wa kanuni na sheria hizo ni Tume Huru ya Uchaguzi ambayo ndiyo msimamizi wa mchakato mzima na inapaswa kuwa huru bila kuingiliwa na mtu, kikundi wala chama chochote cha siasa.

Wahenga wanasema mtu akiumwa na nyoka hata akiona unyasi atashtuka. Hiyo ndiyo hofu ya wapinzani kwamba huenda uchaguzi huo usiwe huru na haki kutokana na historia na kumbukumbu ya mwaka 2020 ambao ulidaiwa kugubikwa na vitimbi vingi na walioshinda kudaiwa hawakushinda bali walipewa tu.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema mambo yote ambayo yana viashiria vya uchaguzi kuwa si huru na wa haki, yakafanyiwa kazi na kila kitu kuwekwa hadharani. Uchaguzi ni kwa mustakabali wa Watanzania wote na si kundi la watu au chama fulani cha siasa, hivyo sheria na kanuni ziwekwe wazi na mchakato mzima uendeshwe kwa misingi ya haki kama ilivyo kwenye sheria.

Pamoja na hayo, demokrasia katika namna yoyote ile imejengwa na misingi kadhaa ikiwamo kuvumiliana baina ya wadau. Kwa hiyo ni vyema kukawa na hali ya kuvumiliana na pale penye tashwishwi au wasiwasi, wahusika wahoji na kupata majibu huku wakitanguliza maslahi ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Denis Mtaita, 0713 578284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vita ya magonjwa yasiyoambukizwa, mazoezi yawe 'lazima si hiari' kwetu



Na Yasmine Protace

**ELIMU** ya kufanya mazoezi kwa jamii, inatakiwa kutolewa kila mara, ili iweze kuisaidia jamii kutopata tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Tena, isiwe elimu tu ya mazoezi, hata ya malazi na vyakula, vyote vikichangia watu kupata magonjwa yasiyo ya kuambukiza, hata jamii nzima ifikiwe na darasa hilo iendelee kutolewa kwa wanajamii.

Serikali nayo imekuwa ikiyataja magonjwa yasiyo ya kuambukiza, jinsi yanavyochangia watu kupoteza maisha huku wengine wakipata ulemavu wa kudumu kupitia magonjwa hayo. Mbali na watu kupoteza maisha au kupata ulemavu, magonjwa hayo, pia yanachangia familia kuyumba kiuchumi, hasa wakati wanawahudumia wagonjwa hao, kutokana na baadhi ya dawa kuuzwa bei kubwa.

Pia, kwa wale ambao figo zao wanasafisha, hali kadhalika wanatumia pesa nyingi kusafisha kila wiki. Kukwepa tishio kwetu la magonjwa hayo, serikali imeanzisha utaratibu wa kuwapo na mazoezi kila Jumamosi kwa ajili ya jamii kutopata magonjwa hayo.

Sasa mazoezi yatafanyika kila wiki, lakini elimu inatakiwa itolewe ili mazoezi hayo yawe endelevu na sio kuyaachia njiani na ikibidi, mazoezi hayo yanapaswa yaanze kufanyika kwa rika zote, kwani hali ilivyo sasa, magonjwa yasiyoambukiza hayachagui rika.

Hivi karibuni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akasema kuwa, ugonjwa wa kisukari na shinikizo la juu la damu (High Blood Pressure) yamo katika kundi la magonjwa 10 yanayowasumbua sana Watanzania.

Katika hilo, anawataka wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha, ikiwamo ulaji wa vyakula pamoja na kufanya mazoezi.

Ni kauli yake waziri baada ya kufanya mazoezi yakiongozwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Jumamosi ya kwanza baada ya kutoa tamko kuwa kila Jumamosi itakuwa siku ya mazoezi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi.

Anasema, kuanzia muda huo wa asubuhi barabara inayoanzia kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dar es Salaam, kupitia daraja la Tanzanite itafungwa kwa maagizo ya serikali ili kupisha watu wanaofanya mazoezi wafanye kwa uhuru.

"Shinikizo la Juu la Damu (High Blood Pressure) pamoja na kisukari ni kati ya magonjwa 10 yanayowasumbua Watanzania, wajibu wetu kama wizara, ni kuhakikisha tunawakinga wananchi wasipate magonjwa.

"Ndio maana tumeiomba serikali kuu kupitia kwa Waziri Mkuu, kufungwe barabara hii ili kupisha mazoezi," anasema.

Anaongeza kuwa, anamshukuru Waziri Mkuu Majaliwa kwa kukubali ombi hilo na kuongoza mazoezi kwa siku ya kwanza baada ya kutoa tamko la kufungwa kwa barabara hiyo kuanzia Taasisi ya Saratani Ocean Road kupitia Daraja la Tanzanite hadi katika viwanja vya Furaha.

Anasema mazoezi yanasaidia sana kukinga magonjwa hususan Kisukari na Shinikizo la Juu la Damu kwa zaidi ya asilimia 50 hivyo wananchi wajitokeze kwa wingi kufanya mazoezi kwa kuwa serikali inatambua umuhimu wa mazoezi.

"Waziri Mkuu nikuahidi, Wizara ya Afya itaendelea kuweka nguvu katika kuwakinga wananchi wako na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kuwahimiza kufanya mazoezi pamoja na kuzingatia mtindo bora wa maisha," anasema Waziri Ummy.

Ummy anatoa shukrani kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam, Albert Chalamila, pamoja na wakuu wa wilaya akiwamo wa Ubungo, Hassan Bomboko, kwa kuweza kuwahamasisha wananchi ambao wamejitokeza kwa wingi kufanya mazoezi.

"Mkuu wa Mkoa nikuahidi, Wizara ya Afya tutaunga mkono vikundi vyote vya mazoezi (jogging) vya mkoa wa Dar es Salaam, tukae pamoja ili tuone mambo gani tunaweza kuyafanya kwa kuboresha ufanyaji wa mazoezi kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi," akatamka Waziri Ummy.

## Ndalichako ashauri mpango mahususi katika kuandaa walimu mkondo wa amali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kasulu Mjini (CCM), Prof. Joyce Ndalichako, ameshauri serikali kuwa na mpango mahsusi wa kuandaa walimu wa mkondo wa amali ili kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa mitaala mipya na kufikia lengo la kuwa na wahitimu wenye ujuzi na umahiri.

Akichangia makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2024/25, Prof. Ndalichako alisema: "Kama mnavyofahamu tulikuwa na elimu ya ufundi na hapa katikati kulikuwa na utaratibu zikawa hazifanyi kazi.

"Kwa hiyo walimu wengi waliondoka kwenda kufanya shughuli zingine. Kwa hiyo serikali iweke mipango Madhubuti ya kupata walimu na hasa ikizingatiwa mwaka 2024/25 serikali ina mpango wa kujenga shule 100 za ufundi na waziri ametwambia wanategemea shule 26 zitaanza kufanya kazi mwaka 2025."

Mbunge huyo ambaye amewahi kuwa Waziri wa Elimu na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), alisema walimu ndio nyenzo na nguzo muhimu katika kuleta ufanisi kwenye mitaala iliyopo kwa sasa.

Aidha, Prof. Ndalichako alishauri serikali iendelee kuajiri na kufanya msawazo wa walimu ili kukabiliana na uhaba wa walimu uliopo.

Alisema utekelezaji wa mtaala mpya utatekeleza umahiri wa vifaa vitakavyowawezesha walimu kutekeleza mafunzo kwa vitendo.

# Othman abeba kero kupeleka kwa Samia

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameahidi kuzibeba kero za Bandari ya Kigoma na kuziwasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan zikiwamo za kukosa sehemu za kufanyia biashara baada ya maeneo yao ya awali kwenye bandari ya Kigoma mjini na Kibirinzi kujaa maji.

Othman ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT Wazalendo, alisema hayo juzi alipotembelea bandari ya Kibirinzi na Kigoma kuona shughuli mbalimbali za biashara, akiwa katika mwendelezo wa ziara yake mkoani hapa ambayo iliambatana na shamrashmra za maadhimisho ya chama hicho kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake .

Taarifa iliyotolewa na kitendo cha habari Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ilisema Othman alisema wafanyabiashara hao wamekumbwa na changamoto kubwa ya kukosa maeneo ya biashara.

Alisema hali hiyo imetokana na maeneo yao waliyokuwa wakiyatumia kwa shughuli za biashara mbalimbali yameingia maji baada ya kina cha maji katika Ziwa Tanganyika kuongezeka na kupanda hadi kwenye masoko ya wafanyabiashara, hivyo shughuli zao kushindwa kuendelea .

Awali, wafanyabiashara hao na wavuvi wanaolitumia Ziwa Tanganyika walimwomba Othman kumweleza Rais Samia kuhusu kero za kukosa masoko na kuomba kutolifunga Ziwa Tanganyika ili kuzuia shughuli za uvuvi kwa miezi mitatu kwa kuwa hatua hiyo itaongeza ukali wa maisha kwa wananchi.

Walisema kwamba masuala kama hayo iwapo yatafanyika, serikali inapaswa kuweka mbadala utakaosaidia wananchi na wafanyabiashara wa eneo hilo kuwa na mazingira sahihi ya kuendelea na shughuli zao za kupata riziki na kujikwamua na ukali wa maisha.

Othman alisema kwamba atamshauri Rais Samia kwamba serikali inaweza kutumia utaratibu wa kutenga maeneo maalumu ya kuzuia uvuvi na mengine kuendelea na shughuli hizo kama kawaida ili wananchi wapate riziki halali kutokana na kazi zao za biashara na uvuvi.

Katika hatua nyingine, Othman aliushauri uongozi wa bandari hizo kufanya jitiada za kutafuta wawekezaji kutokana na kuwapo fursa nyingi zaidi za kusaidia harakati za biashara katika bandari hizo na kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi na taifa kupata maendeleo.


TATEPA
TATEPA PLC

THE COMPANIES ACT, CAP 212 OF THE LAWS OF TANZANIA AS AMENDED COMPANY LIMITED BY SHARES

## NOTICE OF THE ANNUAL GENERAL MEETING

Notice is hereby given that the 30th Annual General Meeting of the Company in respect of the year ended 30th September 2023 will be held at the Coral Beach Hotel Resort, Off Chole Lane, Yacht Club Road, Msasani Peninsula Dar Es Salaam on Thursday of the 30th Of May 2024 at 10:00 East Africa time. To be immediately followed by an Extra Ordinary General Meeting as per separate notice.

1. Confirmation of the minutes of the 29th Annual General Meeting held on Thursday the 27th of April 2023 at the Coral Beach Hotel Resort, Off Chole Lane, Yacht Club Road, Msasani Peninsula Dar Es Salaam at 10:00 AM EAT.
2. To receive, consider and adopt the report of the Board of Directors, the audited financial statements for the year ended 30th September 2023, and the report of the Auditors thereon.
3. To approve payment of no dividend for the year 2023 as recommended by the Board of Directors of the Company
4. Appointment and Re appointment the following Directors for a period of two (2) years:

   a) Mr. George Carmichael Theobald – Chairman
   b) Mr. Robin Harrison
   c) Mr. Alexander Puxley
   d) Mr. Andres De Klerk
   e) Mr. David Bulengo
   f) Mr. Edward Stiles

5. Appointment of Auditors: To re appoint BAKER TILLY DGP & CO, IT Plaza, 10th floor, phone No. +255 653 222 299 Ohio street, Dar Es Salaam as the Company auditors as recommended by the Board of Directors.

6. Any Other Business

A proxy form is attached in hereto and must be lodged at the registered office of the Company not less than 48 hours before the commencement of the meeting.

**BY ORDER OF THE BOARD**

**Rozmin A. Jafferali**
**Company Secretary**
**Tatepa Public Limited Company**
**P.O BOX 700, Tukuyu-Mbeya, Tanzania.**
**Date: 05 May 2024**
**rozmin@tatepa.com**

TATEPA



TATEPA
TATEPA PLC

THE COMPANIES ACT, CAP 212 OF THE LAWS OF TANZANIA AS AMENDED COMPANY LIMITED BY SHARES

## NOTICE OF EXTRAORDINARY GENERAL MEETING

NOTICE IS HEREBY GIVEN to every member of TATEPA PUBLIC LIMITED COMPANY ("the Company), in accordance with Section 134 of The Companies Act, CAP 212 of the Law of the United Republic of Tanzania as amended, that Extraordinary General Meeting ("EGM") of the Company will be held at the Coral Beach Hotel Resort, Off Chole Lane, Yacht Club Road, Msasani Peninsula Dar Es Salaam on Thursday of the 30th May 2024 at 10:15 (EAT) prompt or immediately following the AGM, for the purpose of transacting the following:

**SPECIAL BUSINESS**

1. To consider and if thought fit, pass the following sub-joined resolution as a Special Resolution of the Company:
   (a) That, the Company be and is hereby authorized to sell its 50% shareholding into Wakulima Tea Company ("WTC") to RUNGWE BUSOKELO TEA CO- OPERATIVE JOINT ENTERPRISE ("RUBUTCOJE") on such terms and conditions to be agreed by the parties concerned.
   (b) That, the Board be and is hereby authorized to do all such acts and deeds as well as take all such steps (including but not limited to executing such agreements and documents, appoint professional advisers and other parties, complying with directives of any regulatory authority) which may be incidental, ancillary, supplemental, or otherwise necessary to give full effect to the above resolution and for the aforesaid purpose, on behalf of the Company.

**EXPLANATORY NOTE**

TATEPA PLC owns 1,537,693 shares of each TZS 1,000 equal to 70% of the issued shares in Wakulima Tea Company Limited ("WTC"), a company incorporated in Tanzania with registration no 39757. Whereas TATEPA PLC intends to sell 50% of its shares (equal to 1,098,352 shares of each TZS 1,000) in the company to RUNGWE BUSOKELO TEA CO-OPERATIVE JOINT ENTERPRISE (RUBUTCOJE) which is owned by about 13,838 farmers. After completion of the intended transaction, RUNGWE BUSOKELO TEA CO-OPERATIVE JOINT ENTERPRISE shall own 80% shares in Wakulima Tea Company Limited and TATEPA shall own 20% thereto. Further, upon the intended transaction, TATEPA PLC shall retain its right to lead on governance and control of Wakulima Tea Company Limited by nominating majority Directors pursuant to the Shareholders Agreement dated 6th November 2000 which means that TATEPA shall exercise full control over the Company by influencing relevant board resolutions to be made by the Company.

In light of the above, the Company has convened an EGM to consider, and if thought fit, approve the arrangement and all matters incidental thereto.

Issued by The Order of the Board of Directors on this 5th day of May 2024

**Rozmin Jaferali, Company Secretary,**
**Tatepa Public Limited Company,**
**P.O BOX 700,**
**Tukuyu, Mbeya- Tanzania.**
**Or email to: rozmin@tatepa.com**

TATEPA

# Bajeti TARURA Dodoma yafikia bilioni 66.2/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, bajeti ya matengenezo na ukarabati wa barabara na madaraja kwa mkoa wa Dodoma imeongezeka kutoka Sh. bilioni 12.7 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 66. 2.

Meneja Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Edward Lemelo, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya ofisi yake katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita.

Mhandisi Lemelo alisema ongezeko hilo la bajeti ni kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2023/24 ambalo limeongezeka kwa asilimia 412.77 tangu Rais Samia alipoingia madarakani mwaka 2021.

Pia alisema ongezeko la bajeti hiyo limesaidia kuimarika kwa ubora wa mtandao wa barabara za lami na zege kutoka kilomita 171.29 hadi 309.71 katika kipindi hicho.

"Barabara za changalawe zimeongezeka kutoka kilomita 1,258.65 mwaka 2020/21 hadi kilomita 1,827.5 mwaka 2023/24. Pia madaraja 19, maboksi kalavati 45 na mifereji/ mitaro yenye urefu wa mita 73,822.24 vimejengwa.

"Aidha, taa za barabarani 470 zimesimikwa, barabara mpya zenye urefu wa kilomita 544.60 zimefunguliwa ambazo hazikuwapo kabisa, hii inaakisi kaulimbiu yetu ya tunakufungulia barabara kufika kusiko fikika," alisema Mhandisi Lemelo.

Kadhalika, alisema mtandao wa barabara zenye hali nzuri zimeongezeka kutoka asilimia 10, Februari 2021 hadi kufikia asilimia 34.70 Machi 2024.

Alisema, barabara zenye hali mbaya zimepungua kutoka asilimia 60 Februari 2021 hadi asilimia 31 Machi 2024.

Vile vile, alisema katika kipindi hicho cha miaka mitatu, TARURA mkoa wa Dodoma imeongeza vitendea kazi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi.

"Magari manane mapya yamenunuliwa na kusambazwa katika ofisi za mameneja wa wilaya na mkoa, ununuzi wa mitambo ya ujenzi wa barabara ikiwamo 'Motor Grader', 'Roller', 'Bulldozer' na 'Excuvator' na 'Loadbed' vimenunuliwa na kukabidhiwa kwa meneja wa Wilaya ya Chamwino. Ununuzi wa vitendea kazi umerahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa kazi za wakala," alisisitiza.

Meneja huyo pia alisema idadi ya watumishi imeongezeka kutoka 69 mwaka 2021 hadi 84 mwaka 2024 wakiwamo wa kada ambazo awali hazikuwapo ambazo ni mkaguzi wa ndani, mchumi na ofisa maendeleo ya jamii.

Pia alisema TARURA mkoa imeendelea kutekeleza miradi ya kielelezo ikiwamo ujenzi wa barabara za lami katika mji wa serikali za kilomita 12.6, ujenzi wa barabara ya lami Mwanga - Kisasa - Medelii kilomita 10.7 na barabara ya lami Swaswa - Mpamaa - Arusha Road Jct kilomita 8.2.

Mingine ni ujenzi wa barabara ya lami ya mzunguko Mlimwa kilomita 1.55, barabara katika Soko la Machinga kilomita 0.6 na barabara ya kuzunguka Makazi ya Waziri Mkuu kilomita mbili.



Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Bank of Africa Tanzania, Esther Cecil Maruma (wa tatu kulia), akiwa katika mkutano na Mwenyekiti wa Bodi wa Benki hiyo, Nehemiah Mchechu, kwa ajili ya kujitambulisha na kueleza mikakati ya maendeleo ya benki hiyo. Wengine ni Mkurugenzi wa BoA wa Kanda, Kobby Andah (wa pili kulia), Mratibu wa Huduma za Benki, Hamza Cherkaoui (kushoto), Naibu Mkurugenzi wa BoA Tanzania, Wasia Mushi (kulia) na Meneja Mkuu wa Fedha, Derick Lugemala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kicheko kituo cha afya kupatiwa gari

**Na Munir Shemweta,** MLELE

WANANCHI wa Kibaoni katika Wilaya ya Mlele wameonyesha furaha yao baada ya kituo cha Afya cha Kibaoni kukabidhiwa gari la wagonjwa.

Gari hilo lilikabidhiwa juzi na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ambaye ni Mbunge wa Kavuu, Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi.

Pinda alikabidhi gari hilo katika hafla maalum iliyofanyika eneo la Kibaoni na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Mlele, wakiwamo Mkuu wa wilaya hiyo, Alhaji Majid Mwanga, na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpimbwe, Shamim Daud.

Kukabidhiwa gari hilo kunaifanya Halmashauri ya Mpimbwe kuwa na magari matatu ya kubebea wagonjwa yanayohudumia vituo vya afya vya Kibaoni na Usevya huku gari moja likihudumia Hospitali ya Wilaya ya Tupindo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi gari hilo, Pinda aliwaomba wananchi wa Kibaoni kulitumia kwa manufaa yao huku akimtaka mkurugenzi kuhakikisha gari hilo linabaki kwa matumizi ya kituo hicho na si vinginevyo.

Aliweka wazi kwamba gari hilo litaongeza uwezo wa kituo hicho kwa kuwa mtu akipata rufani kutoka Kibaoni kwenda hospitali ya wilaya, mafuta hayatatumika sana tofauti na awali ilipolazimika mgonjwa kupelekwa Sumbawanga.

Upatikanaji wa gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Kibaoni utasaidia kutatua changamoto za usafiri sambamba na kurahisisha huduma za dharura kwa maeneo jirani kutokana na kuongezeka kwa mahitaji katika eneo la Kibaoni kama vile uwapo wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda.

# Jela miaka 5 kumjeruhi mke kwa panga sehemu za siri

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, imemhukumu Abdallah Mataka (56) mkazi wa kijiji cha Makong'onda wilayani hapa kifungo cha miaka mitano jela baada ya kukutwa na hatia ya kumjeruhi mke wake, Halima Hashim (38) kwa kumcharanga na panga sehemu za siri akimtuhumu kuishi na mwanamume mwingine.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mjini hapa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Batista Kashusha baada ya mahakama kujiridhisha na vielelezo vya ushahidi vilivyotolewa mahakamani hapo na upande wa Jamhuri na upande wa mashtaka.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kashusha alisema kesi hiyo namba 203/2023 ilikuwa na mashahidi watatu ambao walitoa ushahidi wao pasipo shaka, hivyo mahakama imemtia hatiani mshtakiwa kwa mujibu wa sheria kwa kumhukumu kifungo hicho baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa.

Hakimu Kashusha alisema mshtakiwa alifanya kosa hilo na kumjeruhi mke wake kwa kumkata sehemu za siri kwa kutumia panga katika tukio hilo alilifanya Oktoba 8, 2023 majira ya asubuhi akiwa nyumbani kwake.

Alisema mshtakiwa alifika nyumbani majira ya jioni na hakumkuta mke wake akiwa nyumbani ndipo mzozo wa wivu wa mapenzi ulipojitokeza na muda fupi baadaye, Mataka aliingia chumbani na kutoka na panga kisha kumwangusha chini mke wake kuanza kumcharanga, hivyo kumjeruhi vibaya sehemu za siri.

Kashusha alisema hukumu hiyo imezingatia vipengele vyote vya msingi vya kisheria ikiwa ni pamoja na ushahidi wa kitabibu uliotolewa na daktari aliyempatia matibabu mwanamke huyo aliyejeruhiwa.

Awali, Mkuu wa Mashtaka Wilaya ya Masasi ambaye ni Wakili wa Serikali Mwandamizi Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP) Wilaya ya Masasi, Miraji Kajiuli, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia ya kufanya vitendo kama hivyo.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa sababu ni baba wa familia yenye watoto watatu ambao wanamtegemea kimaisha.



## TARI yaanzisha kampeni upandaji miti ya matunda

**Na Steven William,** MUHEZA

KITUO cha Utafiti wa Kilimo cha TARI Mlingano wilayani hapa Mkoa wa Tanga kimeanzisha kampeni ya kuhamasisha upandaji miti ya matunda na mazao ya viungo ili kuimarisha lishe bora nchini na kukabiliana na utapiamlo kwa watoto.

Jana, Mkurugenzi wa Kituo hicho, Catheline Senkoro alisema kuwa kutokana na tatizo la lishe kuwa tishio nchini, TARI imeanza kuwahimiza wananchi kupanda miti hiyo na mazao ya viungo katika mikoa tisa ya Tanzania Bara.

Senkoro, alisema hadi sasa wana miche 16,153 ya miti ya kivuli, mbao, limao, embe, michungwa, migomba, kokoa na mipapai.

"Hiyo miche ya viungo ni mdalasini, karafuu na tangawizi,"alisema Senkoro.

Wakati huo huo; Mbunge wa Muheza na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma ametoa msaada wa majiko ya gesi 135 kwa mama lishe katika vijiji vya Lusanga na Tanganyika.

Akizungumza kabla ya kugawa majiko hayo, Mbunge huyo, alisema ni kwa ajili ya kuwasaidia kuepuka gharama kubwa ya nishati ya mkaa na kuni.

**Mbunge wa Muheza na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma ametoa msaada wa majiko ya gesi 135 kwa mama lishe katika vijiji vya Lusanga na Tanganyika.**

# Diwani, mkandarasi watunishiana misulu mbele ya mbunge Mbise

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

DIWANI wa Kata ya Muriet ya Halmashauri ya Jiji la Arusha, Francis Mbise na mkandarasi wa Kampuni ya Ujenzi ya Hari Singh & Sons Limited, aliyepewa zabuni ya ujenzi wa barabara za kata hiyo kwa kiwango cha changarawe, wametunishiana misuli' hadharani, kisa Sh.600,000 za kuwekewa moramu kutotumika kama walivyokubaliana.

Tukio hilo lilitokea wiki iliyopita mbele ya Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, aliyekuwa amekwenda kwenye kata hiyo kukabidhi gari la wagonjwa la Kituo cha Afya Muriet.

Inaelezwa kwamba Diwani Mbise, alimpa mkandarasi huyo fedha hizo kwa ajili ya kuweka moramu barabarani ili kuharakisha mradi huo wa ujenzi, kitu ambacho hakutekeleza.

"Ninavyoongea hapa, nikimaliza nataka pesa yangu irudi niliyotoa kwa ajili ya kuweka moramu kwenye hii barabara. Baada ya kuona mambo ya ujenzi hayaendi, matokeo yake pesa sioni na kazi haifanyiki.

"Kama mpaka mimi mmenirusha pesa yangu, je, hii barabara itakamilika kwa wakati kweli? Alihoji Mbise, huku akisisitiza kurudishiwa fedha hizo.

Kwa mujibu wa diwani huyo, tangu alipomkabidhi mkandarasi fedha hizo ambazo wananchi wake walichangishana, hakuna kilichofanyika zaidi ya kuwekewa mitambo na kutelekezewa katika barabara.

Alipoulizwa kuhusiana na madai hayo, mkandarasi aliyekuwapo katika eneo hilo la mradi, Stephen Mhauka, alisema aliyechukua fedha hizo kwa Diwani huyo ni mfanyakazi wake, aliyemtaja kwa jina moja la Innocent, huku akiahidi kumtafuta ili arejeshe.

Alisema mkataba wao katika mradi huo, unafikia ukomo Juni 15, mwaka huu, lakini kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, ameomba kuongezwa muda hadi Julai mwaka huu.

Wakati wa majibishano hayo, Gambo alikuwa akiendelea kusikiliza kero za wananchi baada ya kukabidhi gari hilo la wagonjwa kwa kituo hicho cha afya.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' akimkabidhi jiko la gesi mmoja wa wajasiriamali Jestina Hoza, aligawa majiko ya gesi 135 bure kwa mamalishe wilayani hapo katika kijiji cha Lusanga na Tanganyika. Wa tano kushoto ni Mwenyekiti wa UVCCM Muheza, Aziza Mshakangoto. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wafugaji Miti Mirefu washushwa ndoo kichwani

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WATANZANIA wanaokabiliwa na uhaba wa maji wametakiwa kubadili aina ya ubebaji wa vyombo wanavyochotea maji ili kuepuka kupata maradhi ya uti wa ngongo na kibiongo kutokana na kuelemewa na uzito kichwani kwa muda mrefu kwa kutumia madumu yenye magurudumu.

Rai hiyo imetolewa na Rais wa Rotary Club ya Midhurst & Petworth ya Uingereza, John Maguire, wakati akizungumza na wafugaji wa jamii ya Kimasai inayoishi Kata ya Miti Mirefu, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Maguire.

Maguire, alisema baadhi ya nchi za Afrika zimeanza teknolojia mpya ya madumu ya kuburuza badala ya kubeba kichwani ili kuepuka madhara ya kiafya.

Alisema Rotary Club ya Midhurst & Petworth ya Uingereza, Rotary Club ya Kilifi-Kenya, Rotary Club ya Addiscombe & Shirley, Chichester Harbour na E-Club Innovation za Uingereza, zimejitosa kuisaidia jamii hiyo kukabiliana na tatizo hilo kwa kuwapa madumu hayo yenye magurumu.

Rangesh Nallan, Raia wa Singapore ambaye amejitolea kuleta mradi huo nchini baada ya kupanda Mlima Kilimanjaro mwaka 2022, alisema Rotary Club, wanaunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kupitia sera yake ya 'mtue mama ndoo kichwani.'

"Watoto sasa wa jamii hii ya Kimasai wanaweza kwenda shule na akina mama wanawewza kutumia madumu haya yanayotembea bila kusaidiwa kuweka kichwani au kuumia mgongo kwa kubeba dumu la lita 20 mpaka 30 mara tatu hadi nne ili kutosheleza huduma ya maji nyumbani," alisema Rangesh.

Baada ya ugawaji wa vifaa hivyo vya kuburuza, Kiongozi wa mila wa jamii hiyo ya Kimasai (Laigwanani), Michael Laizer, alisema wanaendelea kuiomba Rotary kuwasaidia zaidi kusogezewa huduma ya maji karibu na makazi yao.

"Sisi wafugaji tunapenda kuwashukuru Rotary Club ambao wametusaidia madumu ya kuchotea maji yanayoburuzwa. Wanawake na watoto wa Kimasai katika eneo la Miti Mirefu, wanatembea umbali wa kilomita tano kila siku kwenda kuteka maji Mto Ngarenairobi," alisema na kusisitiza kuwa:

"Kama kuna uwezekano tunawaomba wasichoke kutusaidia tupate maji ya bomba au visima virefu kwa karibu na makazi yetu kwa sababu kinamama na watoto wengi wao ni wanafunzi wanateseka kuamka usiku kwenda kutafuta maji mtoni."

Vilevile, aliiomba serikali iiangalie jamii hiyo kwa jicho la pili kwa kuwapelekea maji karibu na makazi yao kwa kuwa wanakabiliwa na ukosefu wa maji ya bomba na visima.

Sarah Petro, mwanafunzi na mkazi wa Kijiji cha Miti Mirefu alisema: "Tunaomba mtusaidie kwa sababu kuna wazee kule na wanafunzi wanatumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji kiuchumi."

Akifafanua kuhusu teknolojia hiyo, Maulid Mshahame, Mratibu wa Mradi wa Roll Out The Barrel Afrika Mashariki, alisema inatumia mahusus katika vijiji au watu wasiojiweza, wanawake, watoto na jamii ya watu wenye ulemavu.

Alisema madumu hayo yanawaepusha pia watumiaji uzeeni kuepuka maradhi ya kibiongo (kupinda mgongo) na kuathirika uti wa mgongo kwa kubeba madumu mazito ya maji kichwani kwa miaka mingi.



# Kiama wauza mafuta kwenye vidumu

**Na Neema Sawaka,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ( EWURA ) Kanda ya Magharibi, inatarajia kuanza msako wa wafanyabiashara mafuta kwenye vidumu na mapipa hivi kwa kukiuka sheria na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Msako huo ulitangazwa na Meneja wa EWURA wa Kanda hiyo, Walter Chirstopher, wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa ili kudhibiti biashara hiyo na madhara yake katika jamii.

Christopher alisisitiza kuwa wafanyabiashara hao wa mafuta aina ya petrol, disel na taa wanatakiwa kutambua kuwa siku zao zinahesabika na kuonya kuwa wakikamatwa watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya kukiuka sheria za mamlaka hiyo na kuhatarisha maisha ya wananchi kwenye maeneo yao.

"Sheria ya mafuta ya mwaka 2015 kifungu cha 131 inasema mtu yoyote haruhusiwi kuuza mafuta hayo bila kuwa na leseni kutoka EWURA," alisema na kufafanua kuwa: " Masharti ya EWURA mfanyabiashara anayotakiwa kutimiza ni kuwa na leseni na kujenga kituo cha mafuta."

Mhandisi Mwandamizi wa Mafuta wa EWURA, Ibrahimu Kajugusi, alisema mamlaka hiyo imepunguza masharti ya kuanzisha biashara hiyo na kwamba taratibu ziko wazi kwa mfanyabiashara anayetaka gharama za uanzishwaji vituo kwa vijijini zimeainishwa.

"Kwa taarifa ya Aprili 30, mwaka huu tulikuwa na vituo vya mafuta 464 vilivyojenga vijijini nchini nzima kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi na kuondokana na biashara ya kuuza mafuta kwenye chupa za maji ndani ya makazi ya watu, tunaendelea kuweka mazingira wezeshi ili viendelee kujengwa zaidi," alisema.



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Magharibi, Watter Christopher, akitoa elimu kwa waandishi 30 wa Mkoa wa Shinyanga namna Ewura inavyofanyakazi na kudhibiti uchakachuaji wa mafuta kwa kuweka vinasaba, wakati wa mafunzo yaliyofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wazazi wanaoozesha wanafunzi wabanwa

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

KAMATI ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) Kata ya Mwamala mjini hapa imedhibiti utoroshwaji wanafunzi wasichana na kuozwa kinyume cha sheria, imeelezwa.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata hiyo, Sophia Philbert wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na hali ya ukatili katika kata yake kufuatia utekelezaji wa Mradi wa Wanajamii na Vyombo vya Habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ufadhiliwa na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Sophia, alisema wamekuwa wakipata taarifa baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kutoka kwa walimu wakuu wao kuwa hawajulikani walipo hasa wasichana.

Alisema wakuu wao hao, wamekuwa wakifuatulia wanabaini wameozeshwa na wazazi wao kwa kulipwa mahari ya ng'ombe.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Suzana Kayange, alisema wameingia makubaliano ya pamoja ya kukagua umri wa kila anayeolewa kwenye cheti cha kuzaliwa na kadi ya kliniki ili kukabiliana na ndoa na mimba za utotoni ambazo kwa kiwango kikubwa zinakatisha ndoto za wanafunzi kupata elimu.

Alisema kabla ya kuweka utaratibu huo, wasichana wenye umri chini ya miaka 18 walikuwa wakiolewa bila kufuata taratibu kimya kimya baina ya wazazi kwa wazazi baada ya kulipana mahari.

Alisema baada ya utaratibu huo kuanza, hakuna tena ndoa za utotoni na wanafunzi wasichana wanaendelea na masomo.

Mmoja wa wajumbe wa MTAKUWWA, Ramadhani Mahona, alisema ili wawafike wananchi wengi na kuwaelimisha wanatakiwa kuwezeshwa usafiri wa baiskeli na vocha kwa ajili ya mawasiliano ili kupeana taarifa.

## Ulawiti wadhibitiwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VITENDO vya baadhi ya watoto wa kiume kulawiti katika Kata ya Iselamagazi wilayani Shinyanga vimedhibitiwa baada ya watuhumiwa kukamatwa na kuchukuliwa hatua kali.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iselamagazi, Amos Daudi, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu wanavyoshughulika na matukio ya ukatili dhidi ya watoto na wanawake.

Kwa mujibu wa Daudi, kwenye kata hiyo awali kulikuwa na matukio mengi ya ulawiti dhidi ya watoto wa kiume, yakifanywa na watu wazima.

Alisema serikali baada ya kupata taarifa kuhusiana na vitendo hivyo vya kinyama, ilianza kuzifanyia kazi, kuwakamata watuhumiwa na kufikishwa mahakamani.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omary, alitoa wito kwa wazazi kujenga tabia ya kuwachunguza watoto mara kwa mara ili kubaini kama wanafanyiwa vitendo hivyo.

"Kuna mtoto mmoja alianza kulawitiwa akiwa darasa la kwanza na kubainika akiwa darasa la tatu ameharibiwa vibaya sehemu za haja kubwa," alisema Aisha na kuwataka watoto kutoa taarifa za ukatili katika mabaraza ya shuleni ili kutokomeza vitendo hivyo katika jamii.

## Kijana matatani kwa kutaka kujiua

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza linatarajia kumhoji Mwikwabe Range (20) kwa tuhuma za kutaka kujiua kwa kujirusha kwenye daraja la watembea kwa miguu lililopo eneo la Mabatini kwa kinachodaiwa ni kutokana na wivu wa mapenzi.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Wilibroad Mutafungwa alisema kuwa hatua hiyo inafuatia mtuhumiwa huyo kuonekana katika picha ya video iliyosambaa juzi katika mitandao ya kijamii.

Kipande cha picha hiyo kilimuonyesha mtuhumiwa huyo akijirusha katika daraja hilo kwa kile kilichoelezwa kukerwa na kitendo cha mpenzi wake aliyekuwa akimsomesha kugundua kuwa amezaa na mwanamume mwingine.

Mutafungwa, alisema mtuhumiwa huyo, Mkazi wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, alijaribu kujiua kutoka kwenye daraja hilo lenye urefu wa mita 5.5 na kukimbizwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa Sekou-Toure.

"Alijirusha katika kivuko hicho na kuanguka katikati ya barabara Mei 3, 2024 baada ya kumkuta mchumba wake aliyekuwa akimsomesha akiwa na mtoto na mwanamume mwingine na wala hayupo masomoni," alisema kamanda huyo.

Alisema mtuhumiwa huyo alipata majeraha usoni na mikononi na kupelekwa hospitali kwa ajili ya matibabu akiwa chini ya ulinzi wa polisi kwa ajili ya mahojiano.

"Vilevile tunaendelea na upelelezi wa tukio hili utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili," alisema.

Aliwataka wazazi na walezi kuacha kuchukua maamuzi kwa mihemuko bali watafute ushauri kutoka kwa viongozi wao wa dini na watu wenye busara badala ya kutoa uhai kwa maamuzi yasiyo sahihi.

ama
ALHAMISI MEI 9, 2024
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 13

**MUDA KABLA WALIKUWA HAWAJAMBO... Simulizi ya mjamzito apasuliwa kwa mwanga simu, wafa mama na mwana**



**Daktari bingwa achambua wasiyojua watu wengi ndani ya ugonjwa kifafa**

Ukurasa 12

## HOFU 2030 WENYE KANSA KUWA MILIONI...

# Samia vitani; anaingiza darasani Bil. 10/- kila mwaka, zimrejeshee mabingwa 30

### •Ni mwathirika kifamilia, ameanza nayo kitambo

**Na Yasmine Protace**

KUNA shida katika kuongezeka idadi ya wagonjwa wa saratani kila mwaka. Idadi ya wanaobainika kila mwaka ni 40,000 na wanaofariki ni 27,000.

Ni tahadhari inayoleta nakisi inayoongeza idadi ya wagonjwa wa kansa, 13,000 kila mwaka. Hapo inamshtua Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika vita vyake, oneo hilo la kuumba wabobezi na wabobevu wa kupambana nayo.

Kujibu tishio hilo, Rais Dk. Samia anatoa ofa ya 'kuwaumba' mabingwa 30 kila mwaka, Waziri wa Afya. Dk.Ummy Mwalimu, akiwa na ufafanuzi: " Dk. Samia Super-Specialized scholarship Programme imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi ambapo kwa mwaka wa masomo 2023/2024.

"Jumla ya shilingi bilioni 10.9 zimetengwa na kuwawezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi (30 ni wa saratani)."

Kimsingi, Rais Dk. Samia alishafafanua utashi na ushiriki wake katikia vita hivyo miaka sita iliyopita, akiwa Makamu wa Rais, kwamba ukishafikia kwa karibu familia yake.

Hiyo ilikuwa katika uzinduzi wa kampeni vita dhidi ya Saratani ya Mlango wa Kizazi, inayoongoza kwa kuua, kati ya saratani zote, ikiwa tukio la uzinduzi wa chanjo dhidi yake, katika viwanja vya Mbagala Zalheim, Aprili 2018, akitamka: "saratani hii ndiyo iliyomwondoa mama yangu kipenzi.

Mtendaji wake wizarani, Ummy, hadi sasa bado ziko aina nyingi za saratani zinazochukua maisha ya wengi nchini na kwa jumla ya vifo vote, saratani ya mlango wa kizazi ina asilimia 25 ya wote wanaougua saratani, ikifuatiwa na saratani ya matiti yenye asilimia 10.

Ilikuwa kwenye uzinduzi wa Jengo la Huduma za Saratani, katika Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam, lenye uwezo wa kuhudumia wagonjwa 100 kwa siku, mgeni rasmi akiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, wiki iliyopita.



Ndivyo ilivyo tukio, tukio mojawapo la Mwezi wa Uelimishaji Saratani, katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**

Kuhusu mwelekeo wa hali ya saratani nchini, Ummy ana ufafanuzi wa kiserikali:"Vifo vitokanavyo na saratani vitaongezeka ifikapo mwaka 2030, kama hatutachukua hatua za kushughulikia ukubwa wa tatizo hili la saratani nchini, inakadiriwa kufika vifo milioni moja."

**VITA VILIVYOKO**

Waziri anasema, serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea na mapambano dhidi ya saratani, kwamba fedha zimepatikana za kuboresha miundombinu, ununuzi wa vifaa vya kisasa na kusomesha wataalamu katika matibabu ya saratani (mabingwa 30 kila mwaka).

Akifungua Mkutano wa Mwaka wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA) katika ukumbi wa Kinataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, akanena mwaka huu idadi ya madaktari wanaojiendeleza, kuna ziada ya 582, kulinganisha na mwaka uliopita wa masomo.

Anafafanua wanafunzi 79 watasomea udaktari bingwa wa magonjwa ya ndani na kati yao, madaktari 11 sawa na asilimia 33, wameenda kusoma ubingwa bobezi wa magonjwa ya ndani.

Hapo Waziri Ummy anatoa wito kwa madaktari vijana wajitokeze kwa wingi kujiendeleza katika masomo ya ubingwa na ubobezi na wakirudi, wawe tayari kupangiwa vituo vya kazi sehemu yoyote kitaifa, wanakohitajiwa.

"Kupitia muundo huu mpya wa Sekta ya Afya, tutaweza kuwatambua kwa kuwawekea mazingira mazuri madaktari wenye ubobezi katika maeneo mbalimbali, ikiwamo wa masuala ya magonjwa ya ndani," anasema.

Katika mkutano huo, Waziri Ummy akawataka madaktari hao kujadiliana, wao wizarani wapate mapendekezo ya jinsi ya kupunguza magonjwa yasiyoambukiza, kwa kuwa sasa kuna kasi ya ongezeko lake.

Vilevile, Waziri Ummy akawataka madaktari hao kujadiliana na kutoa maoni yao katika mwongozo sahihi wa kitaifa wa matibabu, pamoja na orodha ya taifa ya dawa, ili penye mapungufu yarekebishwa.

"Suala la 'Kitita cha Bima ya Afya NHIF' linatakiwa lijadiliwe kuanzia kwenye mwongozo wa kitaifa wa matibabu, pamoja na orodha ya Taifa ya dawa, tukishakubaliana, tunamwambia NHIF atambue na afuate mabadiliko hayo," anasema.

AFYA

# Daktari bingwa achambua wasiyojua watu wengi ndani ya ugonjwa kifafa

## • Abainisha vyanzo; uvimbe ubongo, hitilafu umeme...

**Na Christina Mwakangale**

WANAOUGUA kifafa wanaelezwa wana hatari ya vifo, mara sita zaidi ya wengine. Tabibu bingwa wa maradhi ya ubongo, Dk. Patience Njenje, anabainisha katika mazungumzo na Nipashe, akitaja mahususi maradhi yako katika kiwango cha asilimia 60.

"Kuwa na kifafa ni hatari. Kifo ni muda wowote...ikilinganishwa na ambao hawaugui ugonjwa huo," anasema bingwa.

Anaendelea kwa ufafanuzi: "Utakuta mtu alikuwa amepanda juu ya mti, akaanguka ghafla, au anaendesha gari, lakini ana kifafa, kinamkamata wakati anaendesha gari, mwendokasi mkubwa, anapata ajali."

Dk. Njenje anasema, ugonjwa huo humkumba anayeugua muda wowote, akitumia mfano wamo waliokuwa wanaogelea, wakadhurika na maji, wakazama na hatimaye kifo.

Kwa mujibu wa daktari huyo, asilimia mkubwa ya wanaougua anawataja ni vijana kuanzia umri wa miaka 15, akibainisha, baadhi yao huangukia kwenye moto na kukosa msaada wa kuwanusuru.

"Mwenye kifafa anaanguka! Akianguka anapoteza fahamu. Anakuwa hajijui. Akiangukia kwenye moto ataungua, akiungua atapata madhara, makovu au ulemavu!

"Asilimia zaidi ya 25 wanaougua kifafa wana ulemavu. Ukiwachukua wote wanaougua milioni 60 duniani, kati yao asilimia 25 wana ulemavu," anafafanua bingwa huyo ambaye anahudumia kliniki ya PCMC, iliyoko Mwenge, Dar es Salaam.

"Watu wanaoishi na kifafa ni zaidi ya watu milioni 60 duniani kote na ni ongezeko la watu 34 hadi 76 kwa kila watu 200,000 kwa mwaka. Kaulimbiu ya mwaka - 2024 ni 'Tulikotoka, tulipo na tunakoelekea."

Anasema, uhalisia huo mwilini anakuwa nao mgonjwa, hata kumjengea vikwazo kimaisha, kwamba: "Huu ni ugonjwa wa kibaolojia. Hizo ni dhana tu. Kwenye ubongo huwa kuna shida, labda kuna uvimbe, hitilafu ya mfumo wa umeme.

"Ikitokea basi mtu atapata shida. Uchawi, mapepo ni imani potofu, ni dhana tu. Asilimia 50 katika jamii watu wanamini kifafa ni ugonjwa wa kuambukiza.

"Kifafa ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza. Mimi mwenyewe nikiwa shule ya bweni nilikuwa nakimbia, niliamini mtu mwenye kifafa akianguka utaambukizwa, tuliamini akijisaidia, akitoa hewa chafu utaambukizwa," anasema.

"Lakini kwa sababu niliendा shule, sasa ninajua, nimeelimika. Kifafa kikikukamata, maana yake, misuli yote inakakamaa, ndio maana mtu anajisaidia, kama tumbo lilijaa ataishia kujisaidia haja ndogo au kubwa."

Anasema, wanaougua pia hunyanyapaliwa, wakikosa tofauti kama vile elimu na wanatengwa na jamii hata familia zao.



Tabibu bingwa, Dk. Patience Njenje wa Dar es Salaam. **CHRITINA MWAKANGALE.**

"Mtu anatakiwa aripoti shule fulani, anaambiwa 'hapana, nenda shule nyingine.' Utakuta mwalimu mkuu (au mkuu wa shule) anakataa, anaonekana ataambukiza watu.

"Kuna unyanyapaa, wengine wanafukuzwa kazi. Lakini ni ugonjwa kama magonjwa mengine, kama kifafa hakiambukizi...kama ni hivyo basi wenye presha, kisukari, saratani wafukuzwe.

"Afrika ni mojawapo, ina asilimia kubwa ya watu wanaoishi na kifafa. Inafahamika ni watu 20-58 kwa kila watu 1,000,' anasema na kuendelea:

"Pia, Tanzania ina idadi kubwa ya wagonjwa wa kifafa katika Afrika na dunia, mojawapo kati ya nchi zenye wagonjwa wengi zaidi."

Bingwa huyo anatumia mifano, kwamba, kwenye vijiji vya Wilaya ya Mahenge, mkoani Morogoro, vina idadi kubwa ya wenye vifaa, wastani wa watu hadi 37, katika kundo la kila watu 1,000, hali inayotajwa kuwafanya watu zaidi ya milioni moja Tanzania, wanaugua.

Kuhusu matibabu, bingwa huyo anasema asilimia tano pekee ndio wanaofika hospitalini, wengi kwenye tiba za kiimani tofauti, kama vile kuombewa makanisani na misikitini, au kwenye tiba za kienyeji.

Mtazamo wake daktari kitalamu ni kwamba, maradhi kifafa kisipewe uhusiano na homa za watoto, ambazo mara nyingi huwasababishia degedege.

Anataja aina ya uhusiano ulioko ni kwamba, panapokuwapo homa kali kwa mtoto, hata kumsababisha apoteze fahamu, ni hatari inayoweza kumsababishia kuwa na kovu kwenye mishipa ya ubongo hatimaye, kifafa.

### HALI ZAO ZILIVYO

Bingwa huyo anaeleza, watoto wenye umri wa kwenda shule wenye tatizo hilo, kwa asilimia 45 hawapelekwi shule. Vilevile, asilimia 68 ya mahudhurio yao hayaridhishi, huku asilimia 37 ndio hupata elimu za msingi.

"Watoto hawa hawaruhusiwi kucheza na wengine, hivyo huhfichwa katika jamii. Asilimia 75 ya wagonjwa huenda kuwaona waganga wa jadi na wengine huenda kuwaona viongozi wa kiroho (dini).

"Kuna watu wengi ambao wana shida ya kifafa kidogo. Sio hadi aanguke, wengine wanapoteza fahamu, wengine wanatikisika tu, labda mkono. Inapotokea kaanguka. usimshikilie, usimzuie, ana hatari ya kufyatuka bega wakati huo.

"Muache ajing'ate, atapona. Usimshikile, mlaze ubavu wa kushoto, asilale chali. Akizinduka mpeleke hospitali," daktari huyo anatafsiri uhalisia na hali ya awali, akiendeleza ufafanuzi kuwa:

"Tunawafundisha pia wagonjwa wa kifafa kwamba, kwanza usiendeshe gari hatujui lini kitakushika, usiogelee, usipande magorofani au majengo marefu, ngazi, asikwee."

Anatoa angalizo kwamba, si kila anayeanguka au kupoteza fahamu, mgonjwa wa kifafa, huku akitoa mbinu za kujikinga na visababishi vinavyozuilika ni kama vile, kumjali mama mjamzito kipindi chote cha ujauzito na kuhudhuria kliniki.

"Ugunduzi na matibabu ya haraka kwa watoto wanapopata homa, kuhimiza choo bora na kwa wale wanaokula nyama ya nguruwe iive, kuacha kuwabagua wagonjwa. Serikali ihakikishe uwapo wa utoaji dawa za kutosha kutibu wagonjwa hawa," anasema.

# TANZANIA KUANZISHA VITUO 2 VIKUU VYA TIBA KINYWA AFRIKA MASHARIKI

**Na Yasmine Protace**

WAKATI kuna juhudi za maboresho kitaalamu, miundombinu na vifaa vikiendelea kuboresha afya nchini, Waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu, anatambulisha wana hatua mpya kiserikali kwa Baraza la Mawaziri wa Kisekta ya Afya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Katika hilo, anasema kuna maombi ya Tanzania kuanzisha vituo viwili vya umahiri kwa Afrika Mashariki vitakavyohudumia afya ya kinywa na meno, pia upandikizaji uloto.

Waziri Ummy ameyasema hayo, kwenye Mkutano wa 24 wa Baraza la Mawaziri wa Kisekta wa Afya wa EAC, uliofanyika mjini Dar ss Salaam, pia ukiwakutanisha makatibu wakuu na manaibu wa wazira husika, kutoka nchi tano za Afrika Mashariki.

"Chuo Kikuu cha Muhimbili kupitia Idara ya Kinywa na Meno, ina wataalamu wa kutosha pamoja na vifaa. Kwa hiyo, tunataka wataalamu wote wa kinywa na meno wa Afrika Mashariki waje Tanzania kujifunza katika taasisi yetu ya MUHAS," anafafanua.

Anasema, hadi sasa Tanzania inafanya vizuri katika masuala ya upandikizaji viungo, ikiwamo upandikizaji wa uloto hususan kwa watoto wenye changamoto za sikoseli.

Nchini kunatajwa ni kati mataifa matano duniani, yenye idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa na shida ya sikoseli.

Anasema, Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), jijini Dodoma, imeshafanya upandikizaji wa uloto kwa watoto 10 wenye tatizo hilo la sikoseli na kati yao, watoto sita wakathibitika kupona ugonjwa huo wa sikoseli.

Waziri Ummy anasema, katika mkutano huo wakaujadili magonjwa ya kuambukiza, Afrika Mashariki kukikabiliwa na changamoto za magonjwa ya malaria, Ukimwi na kifua kikuu.

"Tumeona ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza. Tumeona sasa ipo haja kama Mawaziri wa Afya wa Afrika Mashariki, tuweze kuweka mikakati ya kupambana na magonjwa hayo, ikiwamo kuhamasisha na kuelimisha umuhimu wa kufanya mazoezi," anahitimisha Ummy.

Anasema, siri kubwa ya kuepuka magonjwa hayo ni kuzingatia ulaji wa vyakula, kupunguza unywaji wa pombe na ufanyaji wa mazoezi, kwa Tanzania kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi imetengwa kuwa ni muda wa mazoezi ambapo Waziri Mkuu alitoa agizo la kufungwa na Daraja la Tanzanite kwa muda huo ili kuwapa uhuru watu wanaofanya mazoezi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Kenya, Mary Muthoni, anasema jamii inapaswa kuelimisha juu ya afya kwa kuwa afya inaanzia nyumbani, "usipokata vichaka shida inaanzia nyumbani, usipokula vizuri shida inaanza nyumbani, usipoweka maji safi na salama shida inaanzia nyumbani.

Akizungumza madakatari 1,109 kunufaika na ufadhili wa Rais Samia Suluhu Hassan katika ufadhili wa masomo.

### WAZIRI UMMY ANASEMA KUWA,

Dk. Samia Super-Specialized scholarship Programme imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi ambapo kwa mwaka wa masomo 2023/2024, jumla ya Shilingi 10.9 bilioni zimetengwa na kuwawezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi.

### WAZIRI UMMY ANAYASEMA HAYO,

wakati akifungua mkutano wa Mwaka wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya ndani Tanzania (APHYTA) uliofanyika katika ukumbi wa Kinataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar Es Salaam.

"Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa madaktari bingwa katika kuwaendeleza kitaaluma kupitia programu ambayo imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa kwa mwaka wa masomo 2023/2024, kwa wanafunzi 1,109 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 582 ukilinganisha na mwaka wa masomo 2022/2023," anasema.

Anaongeza kuwa katika idadi ya wanafunzi wote ambao wamepata ufadhili kupitia programu hiyo, wanafunzi 79 watasomea udaktari bingwa wa magonjwa ya ndani na kati yao madaktari 11 sawa na asilimia 33 wamekwenda kusoma ubingwa wa bobezi wa magonjwa ya ndani.

Aidha, Waziri Ummy ametoa wito kwa madaktari vijana kujitokeza kwa wingi kwenda kujiendeleza katika masomo ya ubingwa bobezi hususan kwenye magonjwa ya ndani na wakirudi wakubali kupangiwa sehemu yoyote kwa kuwa mikoa mingine pia inahitaji madaktari bingwa wabobezi.

"Kupitia muundo huu mpya wa Sekta ya Afya, tutaweza kuwatambua kwa kuwawekea mazingira mazuri madaktari wenye ubobezi katika maeneo mbalimbali ikiwemo wa masuala ya magonjwa ya ndani," anasema.

Katika hatua nyingine Waziri Ummy amewataka madaktari hao kujadiliana na kuja na mapendekezo ya jinsi ya kupunguza magonjwa Yasiyoambukiza kwa kuwa kwa sasa kumekuana ongezeko kubwa la magonjwa hayo.

Pia, Waziri Ummy amewataka madaktari hao kujadiliana na kutoa maoni yao katika mwongozo wa kitaifa wa matibabu pamoja na orodha ya Taifa ya dawa ili kama kuna mapungufu yaweze kurekebishwa.

"Suala la kitita cha Bima ya Afya NHIF linatakiwa lijadiliwe kuanzia kwenye mwongozo wa kitaifa wa matibabu pamoja na orodha ya Taifa ya dawa, tukishakbaliana tunamwambia NHIF atambue na afuate mabadiliko hayo." anasema.

AFYA

## MUDA KABLA WALIKUWA HAWAJAMBO...

# Simulizi ya mjamzito apasuliwa kwa mwanga simu, wafa mama na mwana

**Na Mwandishi Wetu**



Mkuu wa hospitali iliyokumbwa na balaa, Dk. Chandrakala Kadam, akihudumia wagonjwa wake.

KATIKA hospitali ya manispaa huko Bhandup, East Upnar, Mumbai, mjamzito alifanyiwa upasuaji wa kujifungua (CS) kwa kutumia mwanga wa tochi ya simu baada ya umeme kukatika. Yeye na mtoto walipoteza maisha kwenye yao kutokana na upasuaji huo.

Familia ya Ansari, ilijiandaa kusherehekea mwaka mmoja wa ndoa na kuzaliwa kwa mtoto, lakini ghafla ikakumbwa na huzuni, ambako matukio ya uzembe wa wauguzi na madaktari umetawala.

Khusruddin Ansari, baba wa mtoto mchanga aliyekufa, akatazama kamera nakusema: "Mtoto anapozaliwa hushuka chini hadi tumboni chini, lakini mtoto wa mkwe wangu alikuwa kifuani na madaktari wawili walikuwa wakijaribu kumsukuma chini kutoka juu.

"Mtoto wetu alikufa tumboni wakati huo. Walimpeleka kwenye chumba cha upasuaji kwa ajili ya upasuaji na kisha wakatoka ili kupata saini ya mwanangu kwenye hati kwani mambo yalienda vibaya.

"Wakati mkwe wangu alipochukuliwa, umeme ulikatika. Lakini waliendelea kumfanyia upasuaji wa kujifungua wakitumia mwangaza wa tochi ya simu . Binti yangu na mjukuu wangu walikuwa tayari wamekufa."

Sahidun na Khusruddin Ansari walikuwa anatarajia kufanya sherehe ya maadhimisho ya kwanza ya harusi yao tarehe 15 Mei

Khusruddin ana mguu mmoja. Familia nzima ya Ansari ilikuwa na furaha kwani ndoa yao ilipangwa baada ya muda mrefu na habari njema ya kupata mtoto ingekuja ndani ya mwaka mmoja.

Katika kipindi cha miezi tisa, wanafamilia wanaeleza kwamba, muda wote anafanyiwa uchunguzi, alikuwa na afya njema.

### MZIZI WA TATIZO

Sahidun Ansari, mwanamke mwenye umri wa miaka 26, mkazi wa Mumbai, alilazwa hospitalino hapo, saa 8. 00 asubuhi Aprili 29 kwa ajili ya kujifungua, daktari akamchunguza mzazi na kusema angejifungua kwa njia ya kawaida.

Hata baada ya saa 12 jioni, harakati hazikusimama, hivyo ndugu walimuuliza daktari tena. Daktari anasema itachukua muda, kwani ni mtoto wa kwanza.

Baada ya muda kusonga, daktari alisema mama na mtoto wako katika hali nzuri na wanazidiwa na maumivu, jamaa na wanapowaomba madaktari kufanya upasuaji wa kujifungua.

Hata hivyo, familia inasema kuwa daktari akasema kuwa uzazi wa asili utafanyika kwa saa moja hadi saa moja na nusu.

Lakini jamaa hao wakaisema kwamba ikiwa ana maumivu, mfanyie upasuaji wa kujifungua. Walidai kuwa daktari hakusema chochote kuhusu hilo.

Wakasimulia, mgonjwa walimpatia chai na biskuti kwa ushauri wa daktari na jioni, kiwango cha moyo wa mtoto kilikuwa 110. Daktari akaahidi wanaweza kuhitimisha uzazi huo kwa njia ya upasuaji.

Rehmunnisa, shangazi wa Sahidun, aliarifu kuwa daktari huyo alimpasua kwa wembe Sahidun, bila ruhusa ya jamaa zake na kumpasua kwa lazima. Damu nyingi ilitoka mwilini mwake.

Anarejea maelezo mengine ya daktari, kwamba kiwango cha moyo wa mtoto kilikuwa pointi 40, hali inayolazimisha kufanyika upasuaji.

Mwili wa mzazi ulivuja damu sana, anasimulia Rehmunnisa akaongeza na baada ya hapo, wakamwambia wampeleke kwenye chumba cha upasuaji.

Anasimulia, hapakuwapo shangazi zake au wauguzi kutoka hospitali hiyo wakati wa kumpeleka huko na nguo yake ilijaa damu.

"Nilipoona haya yote nilikuwa na hofu na nilitokwa na machozi. Daktari aliniomba niondoe nguo yake. Alinipa mkasi wa kurarua nguo yake iliyokuwa imejaa damu.

"Hawakuwa na kiti cha magurudumu au kitanda cha kumpeleka kwenye chumba cha upasuaji. Tukishikilia nguo nyuma yake, tulimbeba hadi kwenye chumba cha upasuaji. Wakati huo huo, umeme wa hospitali ulikatika," anaeleza Rehmunnisa.

Anaendelea: "Sahidun alikuwa na maumivu makali...baada ya upasuaji huo, wakati mtoto wa kiume alipotolewa, baba yake aliitwa na kuambiwa kuwa afya ya kijana huyo ilikuwa mbaya...mtoto alikuwa amekufa, lakini walimficha.

"Baada ya muda walifika na kusema kuwa mtoto huyo amefariki. Baada ya hapo mama huyo alipelekwa hospitali nyingine.'

Inaelezwa, hawakuwa na watu wa kumhamisha mgonjwa kwenye gari la wagonjwa. Ni watu wa familia ndio walifanya kazi hiyo, kwenye gari la wagonjwa hawakuwa na hata hewa ya oksijeni..

"Tulipowauliza, walisema alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kwa kweli, alikufa hospitalini. Hata hivyo, binti yetu alipelekwa katika hospitali ya Sion. Alitangazwa kuwa amekufa huko."

### WENYE MAMLAKA

Ofisa Mkuu wa Afya wa Manispaa Mumbai, Daksha Shah, anasema wameunda kamati ya madaktari 10 wataalamu kutoka hospitali tatu kubwa, wakipewa wiki moja kuwasilisha ripoti, kwa ajili ya hatua kuchukuliwa.

Inaelezwa hospitalini hapo penye mkasa, siku hiyo umeme ulikatika kila mara katika eneo lote na kuhusu mbadala wa kutumia mwanga wa tochi ya simu katika upasuaji, kukifafanuliwa; 1.

"Timu yetu ilishughulikia hali hiyo vizuri. Siku hiyo hiyo, wafanyakazi wetu walitengeneza mwingine wa asili. Tunajaribu kutoa vifaa mbadala wa umeme kwa ajili ya kutoa mwangaza."

Agruti Patil, aliyekuwa mkuu wa idara hiyo penye mkasa, anakiri kumekuwapo na matukio ya uzembe wa madaktari katika hospitali ya Sushma Swaraj Prasrutigriha.

Patil anasema; "Hospitali ya Manispaa haina vifaa. Licha ya malalamiko ya mara kwa mara, hakuna hatua zinazochukuliwa. Nilifika huko saa 12.30 jioni siku ambayo tukio hilo lilitokea na nilikuwa hospitalini hadi saa 4.50 asubuhi.

'Baada ya simu za mara kwa mara, mkuu wa hospitali saa nane na nusu asubuhi, alifika huko. Jenereta katika hospitali haijatumika tangu tarehe 27 Aprili. Pia tumelalamika kuhusu suala hilo kwa serikali."

Jagruti Patil anasema, umeme ulikatika mara saba tangu asubuhi ya siku ya tukio hilo.

Mkuu wa Hospitali hiyo Dk. Chandrakala Kadamm, anakubali makosa hayo ya kiutendaji na ameshawaandikia barua wafanyakazi wake wahusika.

Mhandisi Umeme, Mayur Bhagwat, kutoka idara husika serikalini anakana kuhusika kwamba: wizara yao haihusiki na umeme wa hospitali.'

Anaendelea: "Hatujui nini hasa kilichosababisha kukatika kwa umeme katika eneo hilo na ikiwa jenereta ya hospitali imewashwa au imezimwa."

• *Kwa mujibu wa BBC*




Sehemu ya jengo la hospitali hiyo iliyoko Mumbai, India. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

AFYA

# Wakunga wakusanyika na mambo saba wanayodai kitaaluma, maslahi

**Na Sabato Kasika**

MEI 5 mwaka huu, ilikuwa ni maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani. Kitaifa yalifanyika Dar es Salaam, huku wakunga wakija na maombi saba kwa serikali, katika utekelezaji wa majukumu yao vizuri.

Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Dk. Beatrce Mwilike, akafafaua maombi yao kuwa, wanaitaka serikali iwatengenezee mfumo unaowawezesha wakunga kuwahudumia kinamama na watoto wachanga wakati wa maafa.

Pia apendekeza, haja ya wakunga kujengewa uelewa kuhusu mabadiliko ya tabianchi yaliyvo kwa undani, athari zake kwenye afya ya uzazi, jinsi ya kuwahudumia waathirika na kuzuia matatizo yatokanayo na athari hizo.

Katika ombi la tatu, rais huyo wa TAMAS, ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), akaitaka serikali iongeze idadi ya wakunga kwenye vituo vya kutolea huduma kwa kutoa ajira mahususi kwa wakunga wanaohitimu mafunzo ambao bado hawajaajiriwa.

"Tunaomba mazingira ya kutolea huduma kwa wakunga yaboreshwe zaidi, wajengewe nyumba karibu na vituo vyao vya kazi, kwani huduma zao zinahitaji saa 24, zikiwamo za dharura," anasema Dk. Beatrice.

Rais huyo anataja ombi la tano kuwa wanahitaji kuanzishwa kwa mafunzo ya ualimu wa ukunga ili wahitimu wa ukunga wanaomaliza mafunzo, watoke na ujuzi na stadi za kutosha.

"Vilevile tunaomba kutambuliwa kwa taaluma ya ukunga katika mfumo wa utumishi umma, kwani wakunga wakihitimu, bado wanaajiriwa kwa cheo ofisa muuguzi, kitendo ambacho kinasababisha kupunguza morali ya kufanya kazi," anasema.

Ombi lao la saba kwa serikali, ni kutaka walipwe mishahara na marupurupu mengine kulingana na ngazi zao za elimu, hasa kuanzia ngazi ya wakunga wabobezi.

**UFAFANUZI NAFASI YAO**

Dk. Beatrice anawataja wakunga kuwa 'ni jeshi kubwa na mashujaa wa huduma za afya ya uzazi,' na kwamba jeshi hilo linahitaji kuwezeshwa, ili liweze kutumia mbinu mbalimbali kuwafikia kinamama na watoto popote walipo na kuwapatia huduma wanazohitaji.

"Ni ukweli usiopingika kwamba wanawake na watoto ni waathirika wakubwa wa maafa ya aina zote. Katika wanawake wanaoathirika na maafa, wapo wajawazito wenye uchungu na wengine kwenye arobaini ya uzazi. Wote hawa ni wateja muhimu wa mkunga," anasema.

Anafafanua changamoto kubwa walio nayo, ni jinsi mkunga anavyowafikia walengwa hao, ili wakatoa huduma kipindi hicho cha maafa.

Hapo Dk. Beatrece, anasisitiza kwamba ni muhimu kuwapo mikakati endelevu na madhubuti, ya kuwawezesha wakunga kuwafikia waathirika pale inapohitajika kwa ajili ya kukabiliana na hali hiyo.

"Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni; wakunga ni suluhisho muhimu kwa mabadiliko ya tabianchi', inatukumbusha wajibu wetu kama wakunga kwamba tunahitajika kufanya kazi katika mazingira tofauti yanapotokea mabadiliko ya tabianchi," anasema.

Anasema, kutokana na mabadiliko hayo, kumekuwa na ongezeko la kubwa la joto na kwamba utafiti mbalimbali uliofanyika, umeonyesha kuwa joto kali linaweza kuathiri ujauzito na kuharibika mimba au mama kujifungua kabla ya wakati na kuathiri mtoto atakayezaliwa.

"Wakunga tunapaswa kuwa na uelewa mpana wa mabadiliko hayo ili tupange kutoa huduma kulingana na athari za mabadiliko hayo. Tukumbuke ujauzito, uchungu na kujifungua havijui maafa," anasema.

Rais huyo anaongeza kuwa mikakati hii inaweza kuwa ya kupitia elimu, kuwa na mifumo ya tahadhari na kujiandaa mapema ili kuwalinda watoa huduma na wapokea huduma wakati wote.

"Takwimu za Mwaka 2022 za Umoja wa Mataifa na Shirika la Afya Duniani, zinaonyesha kuwa mkunga mtaalam anaweza kuzuia au kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 70," anasema.

Anasema, iwapo mkunga atapatiwa elimu stahiki, mazingira mazuri na usimamizi mzuri wa kila mara, ku a matarajio watafanya kazi yake vizuri.

Hapo anashauri umuhimu wa kupata ushirikiano wa TAMA, serikali na wadau wengine wa afya ya mama na mtoto.

"Sisi kama chama, tumekuwa tukitoa mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma ili kuwawezesha kuokoa maisha ya mama na mtoto mchanga hasa panatokea dharura," anasema.

Anasema, wamekuwa wakishiriki kikamilifu kampeni ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan ya usimamizi wa huduma za mama na mtoto iitwayo 'Mama Samia Supportive Supervision Campaign'.

**WAKUU SERIKALINI**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, anawaagiza watumishi wa Wizara ya Afya, wadau wa afya kushirikiana ili kuboresha huduma ya afya ya mama na mtoto.

Majaliwa anasema, watumishi wa Wizara ya Afya washirikiane na vyama vya kitaaluma kama Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), kwa kuwa wadau muhimu katika afya.

"Huduma za ukunga zinahitaji ushirikiano kati ya wadau wa afya na jamii kwa ujumla, kwa kuzingatia kuwa kila aliyezaliwa amepitia mkononi mwa mkunga," Waziri Mkuu Majaliwa anasema.

Anasema, njia hiyo itaendelea kusaidia kupunguza idadi ya vifo vya mama wajawazito na watoto vinavyotokea wakati wa kujifungua, kwa kuwa ushirikiano huo umesaidia kupunguza vifo hivyo kutoka 558 mwaka 2015/16 hadi kufikia 104 mwaka 2022.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akahimiza weledi na pia wakunga na wauguzi kuepuka lugha chafu kwa watu wanaohitaji hufuma yao, kwa kuwa kufanya hivyo, ni kuharibu taaluma.

"Fanyeni kazi kwa weledi na kutambua wajibu wenu wa kuimarisha afya za wateja wenu, ili kufanikisha Dira ya 2025 ya Tanzania na Maendeleo Endelevu yenye malengo ya kutoa huduma ya afya ya uzazi inayokidhi mahitaji ya ya afya ya uzazi kwa mama na mtoto," anasema Ummy.

Anafafanua kuwa serikali imeongeza upatikanaji wa huduma za uzazi salama, huduma za uzazi wa mpango, upimaji wa virusi vya Ukimwi kwa wajawazito na upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi.

Waziri Ummy anaongeza kuwa, serikali pia inatoa chanjo kwa rika zote pamoja na elimu ya afya ya uzazi, na kwamba hatua hiyo imesaidia kupunguza vifo vya wajawazito kwa asilimia 80.



Wakunga katika mkusanyiko wao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**





# Washauri mafunzo uokoaji yatolewe kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeombwa kutoa mafunzo maalumu ya mbinu za uokoaji kwa wananchi wa maeneo ya mijini na vijiji ili kusaidia majanga yanapotokea badala ya kusubiri vikosi vya uokoaji kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Ombi hilo limetolewa na wananchi kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe lililotaja kujua waliweza kushiriki kwa kiasi gani katika uokoaji kwenye majanga yanayotokea hapa nchini kama vile mafuriko, ajali, vimbunga na matukio ya moto.

John Samweli mkazi wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, alisema ushiriki wa wananchi kwenye majanga hayo unakuwa hafifu kwasababu wengi hawana mbinu za uokoaji, hali ambayo imekuwa ikisababisha vifo vingi vya watu.

"Wananchi wangekuwa na mafunzo ya mbinu za uokoaji vifo na upotevu wa mali vinavyotokea vingeweza kupungua lakini kwa kuwa wananchi wengi wanakuwa hawana elimu ya uokoaji ndiyo maana maafa yakuwa makubwa," alisema Samweli.

Christopher Awe ambaye ni mkazi wa Kateshi wilayani Hanang' mkoani Manyara alisema kulipotokea janga la maporomoko ya matope wananchi wengi walipoteza maisha na mali zao kwasababu ya vikosi vya uokozi kuchelewa kufika.

Alisema kama wananchi wangekuwa na mbinu za uokoaji na kuwa na vikosi maalum vijijini na mijini vya uokozi vingeweza kusaidia kuokoa watu wengi katika janga hilo.

Atupele Mwakatumbula mkazi wa Majengo jijini Mbeya alisema Tanzania bado iko nyuma katika masuala ya uokozi kunapotokea majanga makubwa ukilinganisha na nchi nyingine.

Alisema mfano katika baadhi ya wilaya hadi sasa hazina hata magari ya zimamoto kiasi kwamba kunapotokea matukio ya nyumba kuwaka moto inakuwa vigumu kuudhibiti, kwamba wananchi ambao nao wanakuwa hawana mbinu za uokoaji wanashiriki kujaribu kuokoa bila mafanikio kutokana na ukosefu wa vitendea kazi.

Hassan Abdallah mkazi wa Mikocheni jijini Dar es Salaam alisema mafuriko yakiyotokea maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Dar es Salaam yametoa somo kwa serikali kuangalia uwezekano wa kutoa mafunzo ya mbinu za uokoaji kwa wananchi.

Alisema wananchi wakipewa mafunzo hayo hata kwa kila mtaa na kuunda kikosi maalum cha uokoaji itasaidi kunapotokea majanga wasaidie kwenye uokoaji kabla ya askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokozi halijafika.

Mwanahamisi Juma mkazi wa Mikindani mkoani Mtwara alisema katika tukio la Kimbunga Hidaya wananchi walikuwa wanapewa taarifa tu kwamba hicho kimbunga kimefika sehemu fulani kina mwendo kadhaa, lakini hawakujulishwa mbinu za kujiokoa kutokana na janga hilo.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alipoulizwa serikali ina mkakati gani madhubuti katika kukabiliana na majanga yanayotokea nchini alisema suala hilo atalitolea ufafanuzi wakati akisoma bajeti ya wizara hiyo Mei 15, 2024.

"Nitatoa ufafanuzi nikisoma bajeti ya wizara hivi karibuni," alisema Masauni katika ujumbe aliomtumia mwandishi wa habari hizi katika mtandao wa WhatsApp.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akitengeneza tofari kwa ajili ya uwekaji wa sehemu ya watembea kwa miguu kwenye zahanati ya Chamwino, mradi ambao unaotekelezwa na wanufaika wa TASAF uliopo Kata ya Chamwino Maili Mbili, Wilaya ya Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Uwanja wa Ndege Msalato kutumika Oktoba mwakani

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

UWANJA wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato mkoani Dodoma ambao utakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa na abiria 1,500,000 kwa mwaka, unatarajiwa kuanza kutumika Oktoba mwakani.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dodoma na Msimamizi wa mradi huo Mhandisi wa Wakala wa Barabara nchini TANROADS, Mahona Luhende, wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari nchini walipotembelea mradi huo.

Alisema mradi huo hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. bilioni 360 ambazo ni mkopo nafuu wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) wakati serikali ya Tanzania ilitoa fidia kwa wananchi waliokuwa wanaishi eneo hilo.

Alisema uwanja huo unajengwa na kampuni mbili za Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd inayojenga majengo ya uwanja huo na Kampuni ya Sinohydro Corporation Ltd inayojenga miundombinu ya barabara.

Alisema mkandarasi wa ujenzi wa majengo ya uwanja huo Beijing Construction alianza ujenzi huo Novemba mwaka 2022 na amefikia asilimia 22.5 na kwamba anatarajiwa kukamilisha ujenzi Oktoba mwaka 2025.

Alisema mkandarasi wa miundombinu ya barabara za uwanja huo amefikia asilimia 56 ya ujenzi.

"Mvua zilizonyesha zilisababisha baadhi ya shughuli kusimama na bila mvua huenda mkandarasi wa majengo ya uwanja angekuwa amefikisha asilimia 60 lakini tunafurahi kuona kwamba mkandarasi wa barabara za uwanja ameshafikia asilimia 56," alisema.

Alisema sehemu ya kurukia na kutua ndege imefikia sehemu nzuri na kwamba wanatarajia mpaka Oktoba mwaka huu baadhi ya ndege zitaanza kupelekwa kutua kama sehemu ya majaribio.

# Askari wanaovujisha siri za wananchi waonywa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, ametoa onyo kwa askari yeyote mkoani hapa atakayebainika kutoa siri anazopewa na raia, kusababisha madhara kwa mtoa taarifa.

Alisema hatua zitazochukuliwa kwa atakayebainika ni pamoja na zile za kinidhamu ikiwamo kufukuzwa kazi.

Alitoa onyo hilo juzi katika kikao alichokiitisha cha wadau wa ulinzi na usalama wa Manispaaa ya Singida kwa ajili ya kujitambulisha kwao baada ya kuripoti mkoani Singida akitokea mkoa wa kipolisi wa Temeke jijini Dar es Salaam.

Kikao hicho ambacho pamoja na mambo mengine kililenga kuweka mikakati ya kuimarisha ulinzi.

Katika kikao hicho kilihudhuriwa na wenyeviti wa serikali za mitaa, viongozi wa vyama vya siasa, madiwani, wafanyabiashara, viongozi wa dini na wa masoko yaliyopo Manispaa ya Singida.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho walidai kuwa wakati mwingine wananchi wanakuwa wagumu kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kutokana na baadhi ya askari wasio waaminifu kuvujisha siri wanazopewa.

Kufuatia hali hiyo, Kamanda Kakwale alisema ili Jeshi la Polisi liweze kupata mafanikio katika utendaji kazi wake askari wanatakiwa kuwa na nidhamu, kutenda haki, weledi na uadilifu.

Alisema tukio la hivi karibuni la walinzi wawili waliouawa maeneo ya Stendi Kuu ya Mabasi Singida lilikuwa ni sawa na Jeshi ka Polisi kupigwa za uso.

Alisema suala la kulinda raia na mali zao ni jukumu la kila mwananchi, hivyo kinachotakiwa ni kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za matukio ya uhalifu.

Kakwale alisema kwa kutambua kuwa Jeshi la Polisi pekee haliwezi kufanya chochote mwaka 2006 lilikuja na mfumo mpya wa ushirikishwaji wa jamii, kuwa na mkakati wa polisi kata lengo likiwa ni kusogea karibu na wananchi.



# Siku 14 watoto 10 wafanyiwa vitendo vya ukatili kijinsia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATOTO 10 wameripotiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kulawitiwa na kubakwa katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, kwa kipindi cha wiki mbili hadi kufikia Aprili 29, mwaka huu.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mji wa Makambako, Masinde Masinde, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema kati ya watoto hao, tisa wamefanyiana wenyewe kwa wenyewe ikiwamo tukio la kaka mwenye umri wa miaka 13 kumbaka mdogo wake mwenye miaka minne, huku mmoja akibakwa na baba yake mzazi.

**Kati ya watoto hao, tisa wamefanyiana wenyewe kwa wenyewe ikiwamo tukio la kaka mwenye umri wa miaka 13 kumbaka mdogo wake mwenye miaka minne.**

"Ni kitu kigumu sana kwenye mji wetu wa Makambako na ukifuatilia mengi wanafanyiana watoto kwa watoto. Wa miaka 13 au 14 anamfanyia labda miaka minne, miaka mitano anamfanyia miaka sita kwa hiyo changamoto inakuja kwamba ni wao wenyewe ndiyo wanafanyiana," alisema Masinde.

Masinde alisema hali hiyo inasababishwa na wazazi kutumia muda mwingi kwenye shughuli za kiuchumi na baadhi ya vijana kuwa na familia mapema licha ya kutokuwa na uwezo wa kuzihudumia.

Mtaalamu wa saikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Iringa, Michael Mistini, alisema ili kukabiliana na matukio ya ulawiti ni lazima wazazi wahakikishe watoto ambao wamefanyiwa vitendo hivyo wapatiwe ushauri wa kisaikolojia ili nao wasiendelee kuwafanyia wengine.

Kwa upande wa baadhi ya wazazi mjini Makambako wakiwemo Evodia Msigwa na Pascal Shauri walisema utandawazi na wazazi kushindwa kukaa karibu na watoto wao ni moja ya sababu kubwa inayosababisha vitendo hivyo kuzidi kuongezeka siku hadi siku.

Evodia Msigwa alisema: "Katika dhambi mbaya ni pamoja na hii ndiyo maana alishuka akaiangamiza Sodoma na Gomola na una kitu nakiona kwamba ndiyo sababu kubwa wa hili tatizo leo hii teknolojia ipo juu sana watoto wetu hawa wanaangalia simu ambayo inataka madudu."



Madaktari Bingwa wa Dk. Samia Suluhu Hassan wameanza kufanya kazi za kitabibu ya kibingwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Njombe (Kibena) mkoani Njombe. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

## Wanafunzi 671 wapatiwa msaada taulo za kike

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WANAFUNZI 671 kutoka Shule ya Sekondari Wanging'ombe mkoani Njombe wanatarajia kuondokana na changamoto ya kukosa taulo za kike wakati wa hedhi baada ya kupatiwa msaada wa taulo za kike za vitambaa.

Msaada huo umetolewa na Shirika la Hust lililopo mjini Njombe, lengo likiwa ni kuwawezesha wanafunzi hao kuhudhuria masomo siku zote.

Akizungumza wakati wa kugawa taulo hizo, Mkuu wa Idara ya Afya na Mazingira kutoka shirika hilo, Faraja Elieza, alisema pamoja na kugawa taulo hizo pia wametoa elimu ya hedhi salama.

"Tumetoa elimu ya hedhi salama na kuzuia ukatili kwa watoto 1,320 pamoja na ugawaji wa taulo za kike za vitambaa za muda mrefu zinazodumu miaka minne," alisema Elieza.

Elieza alisema lengo la ugawaji huo ni kuhakikisha wanapandisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa kike kwa kuwawekea mazingira rafiki pamoja na kufungua milango ya kujiamini.

"Taulo hizo za muda mrefu hutolewa na shirika letu bure ili kusaidia watoto wa kike hasa waliopo kwenye shule za kata ili kuwasaidia waweze kuudhuria masomo vema wawapo katika hedhi ili kufikia ndoto zao," alisema Elieza.

Baadhi ya wanafunzi waliopokea msaada huo akiwamo, Neema Mhesi alisema elimu ya hedhi salama waliyoipata itawasaidia kuwaokoa dhidi ya magonjwa kama fangasi na yale ya mfumo wa mkojo yanayosabishwa na kutozingatia usafi wakati wa hedhi.

"Pia tunashukuru Shirika la Hust kwa msaada wa taulo hizi za muda mrefu utatufanya kuwa nadhifu pamoja na kuongeza muda wa maudhurio ya vipindi vya masomo darasani wakati wote tukiwa hedhi," alisema Mhesi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Wanging'ombe, Frank Nyeregeti, aliitaka jamii kuvunja ukimya juu ya masuala yahusuyo hedhi sambamba na kuepuka unyanyapaa.

Alisema: "Ni mradi unaowalenga baadhi ya wanafunzi wa kike na umeleta tija sana kwa sababu watoto wa kike wamekuwa wakikosa masomo kutokana na hedhi lakini kwa sababu wamepaata kitu cha kujisitiri itasaidia kuwafanya kuudhuria masomo kwa wakati".

## Asilimia sita ya wakazi H/shauri Njombe wanakula mayai

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa asilimia sita ya wakazi wa Halmashauri ya Mji Njombe mkoani Njombe ndiyo wanaokula mayai, huku unywaji wa maziwa ukiwa asilimia 16 jambo ambalo linafifisha jitihada za kupambana na udumavu.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa Ofisa Lishe Halmashauri ya Mji Njombe, Michael Swai, aliyoitoa katika Kongamano la Wanawake la kuwajengea uwezo katika kutokomeza udumavu katika Tarafa ya Njombe Mjini.

Swai alisema wananchi wengi hawatumii mayai na maziwa ilihali ni miongoni mwa vyakula muhimu katika kupambana na udumavu, huku pia mimba za utotoni nazo zikitajwa chanzo cha kuongezeka udumavu na utapiamlo.

"Lakini vile vile katika matumizi ya vyakula tuna asilimia sita tu ya wananchi ndiyo wanatumia mayai na asilimia 16 ndiyo wanatumia maziwa," alisema Swai.

Naye Mratibu wa Huduma za Mama na Mtoto Halmashauri ya Mji Njombe, Grolia Mlowe alisema watoto wengi wanapata ujauzito bila ya kutarajia, hivyo wanajificha bila ya kutoa taarifa na kusababisha kutokupata huduma muhimu.

"Wanatakiwa kufika kwenye vituo vyetu vya afya ili kupata huduma kuhusu uzazi na namna ya kujizuia na ujauzito," alisema Mlowe.

Awali Ofisa Tarafa wa Njombe Mjini, Lilian Nyemele, alisema kongamano hilo limekuja kwa lengo la kutokomeza udumavu, elimu ya ujasiriamali kwa wanawake pamoja na kueleza umuhimu wa matumizi ya bima.

"Kila mtaa wapate kinara wa lishe, kila ubalozi wa nyumba kumi utachagua kinamama wasiopungua watano ili kuwatambua wajawazito walioanza kliniki," alisema Nyemele.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuruthumu Sadick, alisema ili kuweza kuleta tija inapaswa makongamano hayo yafanyike hadi katika maeneo ya vijijini.

Wakizungumza na Nipashe baada ya elimu hiyo mmoja wa wakazi wa mjini Njombe, Vumilia Bange, alisema waamini elimu hiyo inakwenda kuwakomboa watoto wao na kisha kuahidi kuanza kuzingatia malezi na mlo licha ya kuwa bize na majukumu na kutafuta maisha.



## Upungufu wa damu, lishe duni tatizo wajawazito

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UPUNGUFU wa damu na lishe duni bado ni changamoto kwa wajawazito visiwani Zanzibar, kunakosababishwa na kutokula mlo kamili wenye virutubisho ikiwamo mboga na matunda.

Ofisa Uzazi Salama kutoka Kitengo Shirikishi wa Afya ya Mama na Mtoto, Safia Haidhuru Ramadhan, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa asilimia 60 ya wajawazito wanaokwenda kujifungua wanatatizo la upungufu wa damu.

Safia alisema kukosekana kwa damu ya kutosha kwa baadhi ya wajawazito kunachangiwa kwa kiasi kikubwa kukosa mlo kamili wa lishe hasa wanawake wa vijijini.

Alisema hivi sasa kinamama wengi hawazingatii chakula cha lishe kwa kula vyakula vilivyokuwa havina faida katika afya zao ikiwemo ulaji wa chipsi kuku, urojo, udongo na vyakula vyenye mafuta mengi ambavyo havina faida kwa mama na mtoto.

Aidha, alisema mjamzito anapokwenda hospitali akiwa na damu pungufu na akicheleweshwa kufikishwa katika kituo cha afya husababisha kifo. Pia, alisema hali ya vifo kwa wajawazito vitokanavyo na uzazi vimepungua na kwa mwaka 2022 waliripotiwa ni 70 na kwa mwaka 2023 ni 52.

Alisema kupungua kwa vifo hivyo kunatokana na elimu inayotolewa kwa kinamama wakati wanapokwenda kliniki. Alisema licha ya kupungua kwa vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua lakini bado idadi ya vifo vya watoto wachanga imeongezeka na mwaka 2021 hadi 2022 ilikuwa vifo 1,727.

Safia alisema katika kuhakikisha kuwa mtoto mchanga anakuwa salama, kitengo hicho cha afya kinatoa elimu kwa wananchi na wajawazito juu ya kumtunza mtoto kabla ya kuzaliwa na baada ya kujifungua.

# Wasimulia mradi Tuhifadhi Maliasili ulivyowakomboa

**Na Rahma Suleiman,** aliyekuwa Babati

WANAWAKE kutoka vijiji 10 vinavyozunguka Hifadhi ya Buruge WMA wameeleza namna mradi wa 'USAID Tuhifadhi Maliasili' ulivyowakomboa kiuchumi.

Wanawake hao kutoka wilayani Babati mkoani Manyara kwa sasa wamejikita katika kufanya kazi za ujasiriamali na kuachana na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya hifadhi za wanyamapori.

Wakizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) wanawake hao walisema kwa sasa wamejielekeza katika kutengeneza vikapu vya kitamaduni, mikeka, shanga, fagio, majiko sanifu na bidhaa zingine ambapo soko lao kuu ni katika sekta ya utalii.

Walisema kabla ya ufadhili wa mradi huo walikuwa wakijishughulisha na ukataji wa kuni pamoja na kula nyama za wanyamapori.

Lydia Yasfat alisema elimu hiyo imewawezesha kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwamo vikapu na soko lao kuu ni watalii wanaofika katika hifadhi za wanyamapori kwa ajili ya kuangalia wanyama na kujifunza mambo mbalimbali.

Alisema wanawake ni waathirika wakubwa wanaoingia katika migogoro ya ujangili kutokana na kuuziwa nyama zitokanazo na wanyamapori, hali inayowaweka matatani.

"Mimi nimeshakaa gerezani miezi sita kwa kukutwa na nyama ya mnyamapori na wala siyo mimi niliyewinda bali nilinunua tu kwa mmoja wa kijana ambaye aliniuzia kwa ajili ya kupika nyumbani kwangu," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kutoka gerezani alipatiwa elimu ya uhifadhi wa wanyamapori na ujangili na kwasasa amekuwa mfano wa wanawake wenzake na jamii katika kutoa elimu ya uhifadhi.

Ofisa mradi chini ya mradi wa 'Tuhifadhi wa Maliasili' unaotekelezwa na Asilia Giving, Zacharia Laizer, alisema wanawawezesha wananchi hasa wanawake wanaoishi pembezoni mwa hifadhi za taifa kulinda mazingira katika hifadhi hizo.

Alisema baadhi ya shughuli za uhifadhi wanazozifanya kwa kuwashirikisha jamii zinazoishi pembezoni mwa hifadhi hizo ni kuanzisha vikundi vya ujasiriamali na kuviwezesha vikundi hivyo ambavyo asilimia 80 ni wanawake.

Alisema vikundi hivyo ni kutoka katika vijiji vitano vilivyo pembezoni mwa Hifadhi ya Tarangire ikiwamo Ngolley, Vilima Vitatu, Kakoi, Olasiti na Sangaiwe.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema waandishi wa habari wananafasi kubwa katika kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya uhifadhi wa mazingira na hifadhi za wanyamapori ili kuwa na taifa imara lenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira.



Baadhi ya wanawake wajasiriamali wilayani Babati wanaotengeneza vikapu vya utamaduni, waliowezeshwa kupitia Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili ili kuachana na shughuli za uharibifu wa mazingira, wakiwa kando ya barabara kuu itokayo Arusha kwenda Manyara wakiuza bidhaa hizo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kesi za udhalilishaji 471 zaripotiwa ndani ya siku 90

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KESI 471 za udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar zimeripotiwa katika maeneo mbalimbali katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

Hayo yalisemwa na ofisa kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Ramla Hassan Pandu, wakati akiwasilisha mada katika warsha ya usambazaji wa matokeo ya uhamasishaji wa matumizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa asasi za kiraia.

Alisema katika vitendo hivyo 240 ni vya ubakaji, 31 kulawiti, 19 kuingiliwa kinyume na maumbile, shambulio la aibu 50 na kutorosha ni saba.

Ramla alisema bado kuna changamoto ya upatikanaji wa takwimu halisi hasa kwa matokeo hayo kutokana na baadhi ya familia za waathiriwa kumalizana nyumbani.

Alisema licha ya asasi za kirai pamoja na taasisi za serikali kuendelea kutoa elimu katika jamii juu ya kuripoti matukio haya katika vyombo vinavyohusika, lakini bado baadhi ya jamii hawafanyi hivyo.

Ramla alisema kulingana na hali hiyo inaonesha kuwa licha ya jamii kupewa elimu juu ya athari za kutoripoti vitendo vya udhalilishaji, lakini bado hawana hamasa ya kuripoti matukio hayo.

"Tunaona jitihada kubwa zinachukuliwa na taasisi za kiserikali, mashirika na hata hizi taasisi zisizo za serikali lakini bado baadhi ya jamii hawajahamasika kuripoti haya matukio hasa kwa yale yanayafanywa ndani ya familia," alisema.

Ofisa kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Asha Mahmoud, akiwasilisha takwimu za ajali za barabarani kwa miezi mitatu alisema ajali 550 zimeripotiwa.

Alisema chanzo cha ajali hizo mara nyingi zinatokana na uzembe wa madereva kutofauta sheria za barabarani ikiwamo mwendo kasi.

Asha alisema katika takwimu hizo ajali nyingi zimesababishwa na madereva wanaume, huku ajali ambazo zimesababishwa na madereva wanawake zikiwa chache.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Balozi Mohmmed Haji Hamza, alisema takwimu hizo za sensa zitawasaidia taasisi hizo za kiraia katika miradi yao ya kuisaidia jamii.

Alisema kupitia takwimu hizo za idadi ya watu na makazi wataweza kupanga mipango yao kwa mujibu wa mahitaji yanayohitajika katika sehemu husika kulingana na idadi iliyopo.

"Takwimu hizi zitaisaidia serikali katika maendeleo lakini zitawasaidia katika kupanga mipango yenu ya miradi ambayo mnaifanya kupitia mambo mbalimbali," alisema.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema watajitahidi kutoa takwimu za matukio mbalimbali kila mwezi kupitia vyombo vya habari pamoja na mitandao ya ofisi hiyo ili jamii ijue kinachoendelea katika maeneo yao.

Hivyo, aliwataka viongozi wa asasi za kirai kutosita kufika katika ofisini kwake kuchukua takwimu wanazozihitaji kwa ajili ya kufanyia kazi katika mambo yao wanayopanga.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MWAJIBU KHAMISI ZUBERI** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 431823** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/KIN/82899/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ATHUMANI IDDY MWEMZUNDU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3177-0021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIBINDU SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/78488/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BILL THADEUS CHRISPINE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0504/0060** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MRIKE SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/13742/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ROGERS LEONIDAS RWEYONGEZA** Anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE368031** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Tanzania tarehe 26/10/2020, na mwisho wa matumizi yake ni tarehe 25/10/2030. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi au Ofisi ya Idara ya Uhamiaji iliyopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **PHQ/SHI/KAH/2955/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISIHAKA MAULID MTERUKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za Usajili **T 849 DNC** aina ya **MITSUBISHI CANTER,** yenye Chassis No.**FE337B440578,** Engine No.**4D32Z440JC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake! Taarifa ya polisi. **PHQ/SHI/KAH//2981/ 2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KAWE Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Mdai RAHIM MOHAMED**

**Jina la mdaiwa KHALID WARID ADAM**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za Taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: KHALID WARID ADAM**
**KINONDONI DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (eleza hapa habari za madai)
**KWAAJILI YA UTEKELEZAJI WA HUKUMU** kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 mwezi 05 mwaka 2024 saa 03:00 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako ma vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 08 Mwezi 05 Mwaka 2024
Sahihi ya mdaiwa

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

---

**MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SINGIDA**

**MAOMBI NAMBA 21 YA MWAKA 2024**

**ANASTAZIA ALOYCE BUGINGO....................MUOMBAJI**

**VERSUS**

**STANLEY PETER SHIRIMA (Msimamizi wa mirathi ya Peter Shirima) ......................................................MJIBU MAOMBI NA. 1**
**PASCALINA PETER SHIRIMA......................MJIBU MAOMBI NA. 2**
**FREDY PETER SHIRIMA..............................MJIBU MAOMBI NA. 3**
**PENDO PETER SHIRIMA..............................MJIBU MAOMBI NA. 4**
**HAPPY PETER SHIRIMA..............................MJIBU MAOMBI NA. 5**

**KWA: PASCALINA PETER SHIRIMA, FREDY PETER SHIRIMA, PENDO PETER SHIRIMA, HAPPY PETER SHIRIMA – POPOTE MLIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambazo zinaweza kupatikana katika baraza hili. Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria tarehe 22/05/2024 saa 2:00 asubuhi siku ya kutajwa kwa shauri hilo.
**ANGALIA:** kushindwa au kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itaendelea kusikilizwa siku hiyo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Baraza hii leo tarehe 19 Mwezi wa 4 Mwaka 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA
SINGIDA
CHAIRMAN
DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
SINGIDA TANZANIA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 8150 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI**

**RUBENI ENEA MRUTU...........................MAREHEMU**

**JOSEPH MRUTU MOSSES ....................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki jatika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 03 Mwezi JUNI, Mwaka 2024.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 6 Mwezi MEI mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi
Mwanga.

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.6785 OF 2024**

**In the Matter of the Etate of the late ELIMU RAYMOND LYATUU**

**By 1.EVA ELIMU LYATUU**
**2...........................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 23 day of MAY 2023.

Dated at Morogoro this 29 day of APRIL 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.28/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU PAULO EDWARD MSINGWA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ABUBAKARY PAULO MSINGWA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 05 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 03 Mwezi 05 Mwaka 2024.

HAKIMU
PRINCIPAL
PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Dunia yataharuki uvamizi wa Rafah

**GAZA, Palestina**

HALI ya hofu imetanda miongoni mwa Wapalestina tangu Israel ilipotangaza na kuingiza vikosi vyake vya kijeshi katika mji wa Rafah, ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Jeshi la Israel lilisema tayari limedhibiti kituo cha mpakani ambacho kilikuwa kikitumika kuingiza misaada ndani ya Ukanda wa Gaza.

Mpaka wa Rafah ndio pekee wa |Ukanda wa Gaza unaopakana na Misri na umekuwa lango muhimu la kupeleka mahitaji ya kiutu tangu vita vilipoanza Oktoba 7, mwaka jana.

Tangazo la jeshi la Israel kwamba linakidhibiti kivuko cha Rafah lilizusha wasiwasi kwa nchi mbalimbali kiasi cha Rais wa Marekani Joe Biden, kusema hatua hiyo haikubaliki.

Msemaji wa Ikulu ya Marekani, Karine Jean-Pierre aliwaambia waandishi habari kwamba kituo hicho pamoja na vingine ambavyo ripoti zilisema vimefungwa, ni lazima kifunguliwe.

Alisema hiyo inajumuisha kituo kingine cha mpakani cha Kerem Shalom ambacho duru zimearifu kilifungwa jana.

Hata hivyo, kuhusu operesheni ya jeshi la Israel inayofanyika katika mji wa Rafah, serikali ya Marekani ilisema imepatiwa ahadi kutoka serikali ya Israel kwamba itakuwa ya kiwango cha wastani.

Hayo yameelezwa na msemaji wa Baraza la Usalama wa Taifa la Marekani John Kirby, alipozungumza na waandishi habari usiku wa kuamkia jana.

Kwa miezi kadhaa sasa serikali ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, imekuwa ikisisitiza kwamba ni lazima ipeleke wanajeshi wake wa ardhini kwenye mji wa Rafah kukamilisha kile wamekitaja kazi ya kulisambaratisha kundi la Hamas.

Maofisa wa Israel walisema operesheni ya Rafah inalenga kuzuia uingizaji silaha kwenda kwa wapiganaji wa Hamas kupitia Misri na kuharibu miundombinu yote ya kundi hilo ambalo llimeorodheshwa kuwa la kigaidi.

Hata hivyo operesheni hiyo inapingwa kwa sehemu kubwa ya jumuiya ya kimataifa kutokana na ukweli kwamba mji huo ndiyo kimbilio la mwisho kwa mamilioni ya Wapalestina waliojikuta katikati ya mapigano kati ya Israel na Hamas.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, aliitaja siku hiyo majeshi ya Israel walipovamia mji wa Rafah kuwa ya wasiwasi.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ujerumani, Annalena Baerbock, aliitahadharisha nchi ya Israel dhidi ya kufanya operesheni kubwa ya kijeshi kwenye mji wa Rafah akieleza watu milioni moja wa Kipalestina hawawezi kupotelea hewani, akimaanisha idadi hiyo kubwa ya watu wanaweza kuangamia.

Nchi ya Misri, ambayo inaloongoza jitihada ya kumaliza vita, ilisema juzi jioni kwamba pande zote muhimu kwenye mazungumzo ya kusaka amani yanayafofanyika jijini Cairo zimeridhia kurejea mezani kwa mashauriano zaidi.

Hatua hiyo inafuatia upinzani ulioonyeshwa na Israel juu ya rasimu mpya ya makubaliano ya kusitisha vita ambayo kundi la Hamas iliikubali.

Israel kwa upande wake ilisema rasimu hiyo iliyoandaliwa na Misri na Qatar haijatimiza vya kutosha matakwa yake ikiwamo suala la kuachiwa mateka wanaoshikiliwa na Hamas.

Wakati hayo yakijiri, polisi kwenye mataifa kadhaa barani Ulaya walikuwa na kibarua kigumu kuanzia juzi kuvunja maandamano yaliyoandaliwa na wanafunzi wanaowaunga mkono Wapalestina.

Wanafunzi kwenye vyuo vikuu kadhaa nchini Ujerumani, Ufaransa na Uholanzi walipiga kambi kwenye viunga na majengo ya taasisi hizo za elimu ya juu kuonyesha mshikamano na raia wa Kipalestina.

Kwenye mji wa Leipzig nchini Ujerumani kulitokea vurumai kidogo pale polisi walipofika kwenye chuo kikuu kimoja kuwatawanya wanafunzi.

*DW*




Raia wa Palestina waliokuwa wanajihifadhi kwenye mji wa Rafah wakilazimika kuukimbia mji huo baada ya Israel kupeleka wanajeshi wa ardhini kufanya operesheni ya kupambana na Hamas. **PICHA: AFP**



## Kenya kufungua shule Jumatatu

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, William Ruto ametangaza kuwa shule zote zitafunguliwa Jumatatu baada ya nchi hiyo kukabiliwa na mafuriko yaliyosababisha miundombinu mbalimbali kuharibiwa.

Akihutubia wananchi, Rais Ruto alisema ameamua kutoa tarehe ya kufungua shule baada ya kupata ushauri kutoka mamlaka ya utabiri wa hali ya hewa nchini humo.

Wiki iliyopita kiongozi huyo alitangaza kuendelea kufungwa kwa muda usiojulikana kwasababu ya mvua zinazoendelea kunyesha.

Shule zilitakiwa kufunguliwa Mei 6, baada ya tarehe ya awali ya  Aprili 29, mwaka jana ambayo shule zilitakiwa kufunguliwa kusogozwa mbele.

Wakati huo huo, watu 44 wamekumbwa na ugonjwa wa kipindupindu katika kaunti ya Tana River nchini humo.

Taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ilisema maofisa wa Kenya wanaoshirikiana na mashirika mengine wanafuatilia hali ya afya baada ya kutokea mafuriko nchini kote.

Mafuriko hayo yameathiri zaidi ya watu robo milioni huku vifo 238 vimeripotiwa kutokea.

**BBC.**

# Jengo laporomoka, laua 6 Afrika Kusini

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

SERIKALI ya Afrika Kusini, imesema vyombo mbalimbali vimefanikiwa kuwanasua watu 26 kutoka kwenye kifusi cha jengo lililoanguka katika eneo la George, mashariki mwa jiji la Cape Town.

Katika tukio hilo, watu kadhaa wameripotiwa kufa na juhudi zinafanyika kutoka vikosi vya uokoaji vikijaribu kuwapata watu zaidi waliohai ambao bado wamenaswa chini ya kifusi. Hadi kufikia jana jioni watu 27 wameokolewa kutoka kwenye vifusi vya jengo hilo la ghorofa sita ambalo lilikuwa likiendelea kujengwa, sita kati yao wakiwa wamefariki dunia.

Kulingana na mamlaka ya serikali, wakati wa ujenzi huo wafanyakazi 75 walikuwa wakiendeleza ujenzi wa jengo hilo wakati wa tukio hilo.

Shughuli za uokoaji zinaendelea kujaribu kuwaokoa makumi ya watu ambao bado wamekwama kwenye vifusi vya jengo hilo.

Aidha bado haijabainika chanzo cha kuporomoka kwa jengo hilo ambalo lilikuwa na eneo la kuegesha magari katika sehemu ya chini ya jengo hilo.

Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa, ametuma salamu za pole kwa jamaa na marafiki ya waathiriwa wa mkasa huo, huku akitaka uchunguzi ufanyike ili kuepuka matukio mengine kama hayo.

*RFI*

# KOCHA PAMBA ATAKA FUNGU LA USAJILI LIGI KUU MAPEMA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Pamba FC, Renatus Shija, amependekeza uongozi wa klabu hiyo kuanza maandalizi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao mapema kwa kutoa fungu kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya, pamoja na kuwalinda waliopo wasiondoke huku akiwataka mashabiki wa soka Mwanza kuwa watulivu.

Akizungumza juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, baada ya kumalizika mechi maalum ya kuikabidhi KenGold ubingwa wa Championship, kocha huyo alisema Ligi Kuu Tanzania kwa sasa imebadilika kwani ina ushindani mkubwa, hivyo maandalizi ya mapema yanatakiwa ili kuifanya Pamba kuwa timu ya ushindani.

"Tumeshapanda Ligi Kuu, huu sasa siyo wakati wa maneno maneno, wakazi wa Mwanza watulie, Pamba inahitaji maandalizi ya mapema, tunakwenda kwenye Ligi Kuu huko ushindani ni mkubwa zaidi, menejimenti iweke fungu la usajili, pamoja na la kuwalinda wachezaji kwa sababu ushindani ni mkubwa wa kugombea wachezaji.

"Hatuwezi kuingia moja kwa moja na kuweka ushindani mkubwa moja kwa moja, lazima kwanza tuizoee ligi," alisema kocha huyo aliyepandisha Pamba kwa mara ya kwanza baada ya miaka 23.

Katika mechi hiyo, timu hizo ambazo zote zimepanda Ligi Kuu, zilitoka sare ya bao 1-1 na KenGold kupewa kombe lao.

Wakati huo huo, Kocha Kengold, Jumanne Chale ameonekana kuwa na wasiwasi na kibarua chake.

Beki huyo wa zamani wa RTC Kagera, alisema anasikia maneno maneno kuwa huenda asiendelee kuifundisha timu hiyo, badala yake ataletwa kocha mwingine.

"Huenda nisiendelee kuwa katika timu hii, au hata nikiendelea nitakuwa kocha msaidizi, lakini ndiyo soka lilivyo, nakiri kabisa kuwa hayo maneno yapo, lakini hayawezi kunifanya mimi nisiendelee kufundisha soka, mimi najua ninachofanya," alisema kocha huyo.




Wanariadha wa mkoani Mbeya wakishiriki mbio ya 'amsha amsha' jana ikiwa ni maandalizi ya msimu wa saba wa Betika Mbeya Tulia Marathoni itakayofanyika kesho na keshokutwa kwenye uwanja wa Sokoine jijini humo. PICHA: **MPIGA PICHA WETU**

# Betika yalipia washiriki Mbeya Tulia Marathon

**Mwandishi Wetu**

WAKATI wanariadha nchini wakihesabu saa za kuanza kusaka medali za msimu wa saba wa mbio ya 'Betika Mbeya Tulia Marathoni' kesho na keshokutwa, wadhamini wakuu wa mbio hizo wamewagharamia watu wote waliojitokeza jana kwenye amsha amsha ya maandalizi ya kushiriki mashindano hayo.

Washiriki 420 kutoka jijini Mbeya jana walishiriki mbio maalumu ya 'amsha amsha' ikiwa ni sehemu ya maandalizi kujiweka fiti tayari kukimbia kwenye msimu wa saba wa Betika Mbeya Tulia Marathoni itakayofanyika kwenye uwanja wa Sokoine.

Amsha amsha hiyo ambayo haijawahi kutokea katika mbio nyingi nchini ilianzia kwenye eneo la Ruandanzovwe hadi kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Beno Malisa ambaye aliwakabidhi bendera ya Twende kibingwa washiriki wa mkoa huo ambao kati yao, 420 watagharamiwa na Betika kushiriki marathoni hiyo kubwa nchini.

Hamasa ya mbio hiyo maalumu kwa ajili ya kukusanya fedha ili kuboresha miundombinu ya afya na elimu jijini Mbeya na mikoa jirani imefanyika kwa wiki kadhaa ikiwamo jijini Mbeya kwa siku nne mfululizo kuanzia Jumapili iliyopita.

Mikoa mingine iliyofanyika ni Morogoro ambako iliongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, Dodoma iliongozwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Dar es Salaam iliongozwa na Naibu Waziri wa Michezo, Hamis Mwinjuma (Mwana FA).

Mikoa mingine ambako amsha amsha ilifanyika ni Rukwa ambako iliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Nyakiya Chilukile, Newala iliongozwa na Meya wa Newala, Hamis Namata na Iringa iliongozwa na Meya wa Iringa, Ibrahim Gwada na waliofanya vizuri kwenye mikoa hiyo wamegharamiwa kwenda kuchuana jijini Mbeya kesho na keshokutwa.

Akizungumza jana, Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvenalius, alisema kuanzia leo wataanza kupokea washiriki kutoka nje ya Mkoa wa Mbeya ili kuungana na wenyeji ambao kampuni hiyo itawagharamia gharama zote za kushiriki mbio hizo msimu huu.

"Kama wadhamini wakuu, pamoja na mambo mengine tumeamua kuongeza hamasa hii kwa washiriki ili kuwapa fursa kuonyesha vipaji vyao," alisema Rugambwa. Washiriki hao watakimbia mbio ndefu za barabarani za kilomita 10, 21 na 42 zinazofanyika Jumamosi zikitanguliwa na zile za mita 100, 200, 400, 800 na 1,500 zitakazofanyika kesho Ijumaa kwenye Uwanja wa Sokoine.

Katika mbio hizo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwaongoza wakimbiaji zaidi ya 5,000 kusaka mabingwa wa marathoni (kilomita 42), nusu marathoni (kilomita 21) na kilomita 10.

Miongoni mwa wanariadha maarufu watakaoshiriki katika mbio hizo ni Sarah Ramadhan ambaye kwa mujibu wa kocha wake, Amani Ngoka mbali na kusaka medali ya dhahabu, ataitumia mbio hizo kama sehemu ya kujipima kasi na kuwa moja ya maandalizi ya kutafuta viwango vya kushiriki mashindano yajayo ya dunia.

Ofisa Habari wa Taasisi ya Tulia Trust wanaoandaa mbio hizo, Joshua Edward alisema maandalizi yako katika hatua za mwisho na tayari baadhi ya washiriki wameanza kuwasili jijini Mbeya.

## Fei Toto: Sishindani na mtu kwenye kufunga

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Azam FC, Feisal Salum 'Feitoto' amesema kila anachokifanya uwanjani ni kwa ajili ya timu yake na anapofunga hakuna anayeshindana naye bali ni kuipa matokeo mazuri timu yake.

Nyota huyo amesema anafurahi kuona anaisaidia zaidi timu yake kuweza kupata matokeo mazuri katika kila mchezo.

Azam leo inashuka uwanjani kuumana na Simba kwenye mfululizo wa michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayokwenda ukingoni.

"Kila ninachokifanya uwanjani ni kwa ajili ya timu yangu, sichezi kwa kushindana na mtu nacheza kuisaidia timu kufanya vizuri, nashukuru Mungu kwa kila kitu kizuri ninachokifanya kwa ajili ya timu, ushindi tunaopata niwe nimefunga mimi au mtu mwingine unatokana na jitihada na juhudi za wachezaji wote," alisema Feitoto.

Feitoto mpaka sasa ameifungia timu yake mabao 15 na kutoa pasi za magoli 'asisit' saba akilingana na kiungo wa Yanga, Azizi Kii.

Mashabiki wa soka nchini tayari wameanza kuwashindanisha nyota huyo kutokana na kasi yao ya kufunga huku wakiwa wamelingana idadi ya mabao ya kufunga na wanaamini mfungaji bora msimu huu atatoka kati yao.

## Simba yataka pointi 3 kwa Bunda Queens

**Na Saada Akida**

VINARA wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, Simba Queens, wanashuka dimbani leo kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya Bunda Queens mchezo utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex saa 10:00 jioni.

Simba Queens inayoongoza ligi hiyo imejipanga vizuri kuhakikisha wanaendelea walipoishi kwa kushinda kila mechi iliyopo mbele yao kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kutaka kumaliza ligi bila kupoteza.

Akizungumzia mchezo huo Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema kazi kubwa ya maandalizi waliifanya mwanzoni mwa msimu muda huu anasahihisha makosa yanayojitokeza katika mchezo uliopita.

Alisema wachezaji wake wapo tayari kupambana kwenye mchezo huo ili kusaka alama tatu muhimu ili kuyafikia malengo yao ya kutaka kushinda mechi zote za mzunguko wa pili.

## ZISIKUPITE

### TEN HAG BADO YUPO
KLABU ya Manchester United haina nia ya kumfukuza kocha Erik ten Hag kabla ya fainali ya Kombe la FA Mei 25. ***(Telegraph)***

### TUCHEL AITAKA BAYERN
KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel ana nia ya kuwa kocha wa Manchester United iwapo klabu hiyo itaamua kumfukuza Erik Ten Hag. ***(Telegraph)***

### MOURINHO NAE AITAKA
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho angependa kurejea kwa kipindi cha pili lakini klabu hiyo haitaki kumteua tena Mreno huyo mwenye umri wa miaka 61, ambaye alitimuliwa na Roma Januari. ***(Manchester Evening News)***

### MARC GUEHI KUUZWA
KLABU ya Crystal Palace iko tayari kumuuza mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23, badala ya kumtoa winga wa Ufaransa Michael Olise mwenye miaka 22, au winga wa Uingereza Eberechi Eze mwenye miaka 25, msimu huu. ***(Givemesport)***

### GASSOVA ATAKIWA
WEST Ham imeanza mazungumzo ya kumsajili winga wa Corinthians mwenye umri wa miaka 19 raia wa Brazil, Wesley Gassova, ambaye analengwa na Liverpool. ***(Standard)***

### CHELSEA KUMUUZA BROJA
CHELSEA inatafuta mnunuzi wa mshambuliaji wa Albania, Armando Broja kufuatia kipindi cha mkopo cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kwenye klabu ya Fulham. ***(Fabrizio Romano)***

### CHELSEA YAMUWINDA WILLIAN
CHELSEA ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili winga, Estevao Willian mwenye umri wa miaka 17 kutoka Palmeiras. ***(Mail)***

### PICKFORD AWINDWA ENGLAND
CHELSEA pia wamemtambua mlinda mlango wa Everton, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 30 kama wanayemlenga majira ya joto. ***(Football Insider)***

### KELLY HUYO NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 25. ***(Foot Mercado)***

### HALL ATAKIWA B. DORTMUND
MLINZI wa kushoto wa Newcastle United, Lewis Hall mwenye miaka 19, ameibuka kama nyota anayelengwa na Borussia Dortmund msimu wa joto. ***(Givemesport)***

### LAPORTA AMTAKA GREENWOOD
RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amewasiliana na Getafe kuhusiana na hali ya mshambuliaji wa Manchester United Mwingereza anayecheza kwa mkopo, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22. ***(Radio Marca)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MARCO REUS APAGAWA DORTMUND KUTINGA FAINALI

Asema ni furaha isiyoelezeka kucheza hatua hiyo baada ya miaka ...

**PARIS, Ufaransa**

MARCO Reus aliita kurejea kwake kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya miaka 11 akiwa na Borussia Dortmund "haielezeki" wakati timu yake ilipoishinda PSG kwa jumla ya mabao 2-0.

Mats Hummels alifunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 mjini Paris siku ya Jumanne na kutinga fainali hiyo itakayopigwa Juni 1 huko London.

Mnamo 2013, Reus alipoteza kwa 2-1 dhidi ya Bayern katika fainali akiwa na Dortmund iliyokuwa na nyota Robert Lewandowski na Ilkay Gündogan chini ya Kocha Jurgen Klopp.

Shujaa wa Jumanne usiku Hummels pia alikuwa mchezaji mwenza wa Reus' mwaka 2013.

"Haielezeki. Baada ya zaidi ya miaka 10, niko kwenye fainali na Borussia tena," alisema Reus, ambaye anaiacha timu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

"Jinsi tulivyoshinda mchezo, hakuna atakayeuliza. Cha muhimu ni kwamba Borussia Dortmund iko kwenye fainali tena."

Reus aliingia uwanjani muda mfupi baada ya Hummels kufunga bao lake la kichwa kutokana na krosi ya Florian Wirtz na kuisaidia Dortmund kupata ushindi wa pili wa bao 1-0 dhidi ya mabingwa hao wa Ligue 1.

"Leo (juzi) ilikuwa wazi kwamba tulihitaji kuteseka na kwamba tulihitaji bahati, lakini walichofanya wachezaji wenzangu ni wazimu," aliongeza Reus kwa furaha.

HABARI MICHEZO

# MBAPPÉ: NILAUMIWE MIMI PSG KUTOLEWA UEFA

**PARIS, Ufaransa**

MCHEZAJI nyota wa PSG, Kylian Mbappé, anapata sifa timu yake inaposhinda, lakini ameamua kubeba lawama baada ya kutolewa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alisema kufungwa kwa timu yake na Borussia Dortmund katika nusu fainali hiyo kwa jumla ya mabao 2-0 yeye anapaswa kubeba lawama.

"Nilijaribu kuisaidia timu yangu kadri nilivyoweza lakini sikufanya vya kutosha," alisema Mbappé baada ya mechi hiyo iliyochezwa Parc des Princes.

"Unapoongelea kuwa na ufanisi kwenye uwanja nadhani mimi ndiye ninayelengwa, mimi ndiye ninayepaswa kufunga mabao na kuwa na maamuzi. Mambo yanapokuwa mazuri huwa najitangaza na yanapokuwa sivyo nawajibika.

"Wa kwanza ambaye alipaswa kufunga leo (juzi) usiku ni mimi. Hayo ndiyo maisha na tunapaswa kusonga mbele, mimi na timu," alisema Mbappe.

Wakiwa na umiliki wa takriban asilimia 70 na mashuti 30 katika mechi hiyo, mabingwa hao wa Ligue 1 waligonga mwamba wa goli mara nne na kutoka mikono mitupu, lakini Mbappé alisema PSG walikuwa na bahati mbaya.

"Sijui kama walikuwa bora kuliko sisi. Hatuhitaji kuwadharau," alisema Mbappé.

„Kwa maoni yangu walikuwa bora. Walikuja mara moja au mbili kwenye lango letu na wakafunga. Mara nyingi tulikwenda kwao na hatukufanikiwa kufunga. Ni ukweli," alisema Mbappe.

Dortmund walifunga mapema katika kipindi cha pili kupitia kwa Mats Hummels na kufanya kazi nzuri ya kumzuia Mbappé.

Huenda huo ulikuwa mchezo wa mwisho wa Mbappé wa Ligi ya Mabingwa akiwa na PSG, huku mshindi huyo wa Kombe la Dunia akitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

Lakini alipoulizwa kuhusu taarifa yake ya kuhamia Real Madrid msimu huu wa joto, Mbappé aliwakodolea macho waandishi wa habari na kuondoka.

"Sidhani tulikuwa duni katika mechi zote mbili," kocha wa PSG, Luis Enrique alisema.

"Matokeo ndivyo yalivyo na ninawapongeza na kuwatakia kila la heri kwa ajili ya fainali, kwa upande wetu tunahitaji kupona kipigo hiki kizito.

"Ni wakati wa huzuni unapopoteza na haswa kwa njia hii. Nawapongeza Borussia," alisema kocha huyo.

Dortmund iko mbioni kunyakua taji lao la pili la Ligi ya Mabingwa baada ya kushinda 1997, wakati kwa PSG ni msimu mwingine unaomalizika bila kuinua taji ambalo wamiliki wao wa Qatar wanalitamani.

"Wachezaji na kocha walijitolea kwa kila kitu. Hongera kwa Dortmund, tulistahili. Ni mchezo mgumu. Ninajivunia timu yangu, changa zaidi barani Ulaya," Rais wa PSG Nasser al-Khelaifi alisema.




## Silva anaweka tarehe ya mwisho kuondoka City

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Kati wa Manchester City, Bernardo Silva, anataka mustakabali wake utatuliwe ifikapo mwisho wa Euro 2024 huku akihusishwa na Barcelona.

Silva mwenye umri wa miaka 29 amefurahia maisha mazuri akiwa Man City, akishinda mataji matano ya Ligi Kuu, mawili ya Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa kwenye Uwanja wa Etihad.

Alihamia Ligi Kuu England mwaka 2017 baada ya kufurahia muda katika Liga ya Ureno akiwa na Benfica kabla ya muda mfupi wa Ligue 1 akiwa na Monaco.

Baada ya miaka saba ya mafanikio chini ya Pep Guardiola, Silva anasemekana kutaka changamoto mpya.

Kujiunga na Barca kunaweza kumfanya kiungo huyo kuhusishwa na wachezaji wenzake wa Ureno na walioko kwa mkopo kwa sasa Joao Cancelo na Joao Felix - ambaye amedai Silva ameonesha nia ya kuhamia Katalunya na Ilkay Gundogan, mshirika wa zamani wa City.

Hapo awali iliripotiwa kwamba Silva anapenda Barcelona kama jiji na „ana kichaa" juu ya kujiunga na klabu hiyo wakati fulani katika siku zijazo.

Hata hivyo, Silva hatasubiri hadi siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho ili kujua mustakabali wake uko wapi, kwa mujibu wa Sport.

Ripoti inadai Silva anataka kujua klabu yake ijayo kabla ya mwisho wa Euro 2024, na kufanya tarehe 14 Julai kuwa mwisho wake.

Wakati huu wa mwisho utamruhusu Silva kufurahia utulivu baada ya mchuano bila kuwa na wasiwasi kuhusu hatima yake ijayo. Inaweza pia kumruhusu kushiriki katika michezo ya kabla ya msimu mpya kwa klabu yake mpya.

Kocha wa Barca, Xavi amekuwa akimpenda mchezaji huyo na atasalia kwa msimu mwingine baada ya kubadilisha umuzi wake wa kuondoka mwishoni mwa kampeni ya sasa.

Matatizo ya kifedha ya Barca yanamaanisha kwamba watalazimika kuuza wachezaji kabla ya kuweza kusajili msimu huu wa joto.

Pia wamehusishwa na nyota wa Liverpool, Darwin Nunez kama mbadala wa mshambuliaji Robert Lewandowski.




## Man United haina haraka na Ten Hag

**MANCHESTER, England**

WAMILIKI wa Manchester United watachukua muda wao kabla ya kufanya uamuzi kuhusu hatima ya Erik ten Hag, vyanzo vimeiambia ESPN.

Nafasi ya Ten Hag kama kocha ipo hatarini kufuatia msimu mbaya, lakini mmiliki mwenza mpya Sir Jim Ratcliffe na timu yake ya INEOS wameendelea kupanga Mholanzi huyo kuwa mkufunzi mpaka fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City Mei 25.

Hata hivyo, kuna kukubalika kwamba kichapo cha aibu cha Jumatatu cha 4-0 dhidi ya Crystal Palace kimemwacha kocha huyo wa zamani wa Ajax mwenye umri wa miaka 54 kuwa hatarini zaidi.

Timu mpya ya uongozi wa soka ikiwa ni pamoja na mkurugenzi mpya wa ufundi Jason Wilcox, hawataki kufanya uamuzi „wa hofu" licha ya shinikizo kuongezeka.

Ten Hag ana mkataba Old Trafford hadi 2025, lakini hajapewa hakikisho rasmi kwamba atakuwapo msimu ujao.

Kuna hofu ndani ya klabu hiyo kwamba, baada ya United kuporomoka hadi nafasi ya nane, kiwango cha timu hiyo ni kibovu kiasi cha kuhatarisha aibu zaidi katika michezo yao iliyosalia ya ligi.

United itamenyana na Arsenal, Newcastle United na Brighton kwenye Ligi Kuu kabla ya kampeni kuisha kwa fainali ya kombe la FA dhidi ya Man City kwenye Uwanja wa Wembley.

Watalazimika kumaliza angalau nafasi ya saba, au kushinda Kombe la FA, ili kupata nafasi ya kucheza Ulaya msimu ujao.

Matumaini ya kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya tayari yametoweka, lakini nafasi ya kucheza Ligi ya Europa au Ligi ya Europa Conference itatoa fedha muhimu na kupunguza shinikizo la kifedha la klabu kabla ya dirisha la usajili.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba kuna huruma kwa Ten Hag, ambaye alilazimika kuchezesha kikosi cha pili dhidi ya Crystal Palace wakati anashughulikia orodha ndefu ya majeruhi, lakini pia kuna hisia kwamba maonesho ya hivi karibuni yamekuwa ya kutisha sana.

United wameshinda mechi mbili pekee kati ya 10 zilizopita za Ligi kuu, wakiruhusu mabao 21 katika mchakato huo.

Bayern Munich wameonyesha nia ya kutaka Ten Hag awe kocha wao mpya, lakini amewaambia wababe hao wa Ujerumani anapendelea kubaki United. Bayern wanatafuta kocha mpya kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel, ambaye ataondoka Allianz Arena mwishoni mwa msimu huu.

**HABARI MICHEZO**

# DEWJI SASA KUSIMAMIA MWENYEWE USAJILI SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

MWEKEZAJI na Rais wa Heshima wa Klabu ya Simba, Mohamed Dewji, anatarajiwa kuwa sehemu ya wafanya uamuzi ndani ya klabu ya Simba ikiwa pamoja na kusimamia usajili wa wachezaji kuelekea msimu ujao wa mashindano, imefahamika.

Habari za ndani ya klabu hiyo zinasema inatarajia kuandaa muundo mpya ambapo Dewji atakuwa sehemu ya watoa uamuzi wa mambo mbalimbali ikiwa pamoja na usajili wa wachezaji watakaoidhinishwa na benchi la ufundi.

Taarifa zinasema hali hiyo inakuja kufuatia kile kilichoelezwa klabu hiyo imekuwa haifanyi vizuri kwenye madirisha ya usajili kwa siku za karibuni.

Imeelezwa uongozi umekuwa ukileta wachezaji wengi ambao hawakidhi viwango vya kuichezea klabu hiyo kitu ambacho hata mwenyewe (Dewji) amekuwa akikilalamikia.

Taarifa zinaenda mbali zaidi na kusema Simba imekuwa haifanyi vizuri kwenye usajili tangu Dewji alipoondoka katika nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, imekuwa ikisuasua katika masuala ya usajili kiasi cha kutegemea wachezaji wale wale wa zamani huku idadi kubwa ya wageni wakionekana kuwa na uwezo wa kawaida.

„Hivi sasa klabu inaandaa muundo mpya kuelekea msimu ujao, Dewji atahusika kwa karibu zaidi na timu kuliko hapo awali, yaani atawekwa karibu zaidi katika mambo yanayoihusu klabu.

„Sasa atakuwa sehemu ya uamuzi utakaokuwa unachukuliwa kwenye klabu ikiwa ni pamoja na kufuatilia usajili wa wachezaji wapya, hii ina maana atakuwa anafuatilia kila kitu kinachofanyika au kutokea, kwa sababu ya haya yanayotokea. Timu haifanyi vizuri, misimu mitatu sasa sawa na madirisha sita ya usajili, wachezaji wanaoletwa wako chini ya kiwango cha kuichezea klabu kubwa kama hii, hivi sasa kuna kelele za mashabiki wa Simba nchi nzima, watu hawaendi viwanjani, haya yote yamesababisha haya mabadiliko, lengo ni kuirudisha Simba ile ambayo watu wameizoea," kilisema chanzo hicho.

Katika hatua nyingine, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba amesema kwa sasa akili yao wameielekeza kusaka nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao na si kingine.

Alisema mambo yote ya klabu, ikiwemo usajili yatajulikana baada ya msimu kumalizika.

„Nadhani kwa sasa Wanasimba tunapaswa tushirikiane ili tumalize ligi salama na kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

„Baada ya hapo tutakwenda kukaa chini sisi kama viongozi wa Simba na kuangalia nini tufanye, wapi turekebishe, lakini kwa kuwa timu yetu msimu huu haijafanya vizuri, maana yake tuna wajibu wa kufanya maboresho makubwa ili tuwe na msimu ujao mzuri.

„Kama jahazi linayumba, kuna mambo mawili, kwanza kupunguza mizigo ili likae sawa, au ugeuze, urudi pwani ili ujipange upya, kwa hiyo sisi kuna mambo tutayafanya ili kujiweka vizuri, sisi kama viongozi tunajua nini cha kufanya kuelekea msimu ujao," alisema Ahmed.



Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (katikati), akimvalisha medali mmoja wa wachezaji wa timu ya Kengold baada ya kuibuka vinara wa Ligi Daraja la Kwanza 'Championship' katika hafla iliyofanyika jana Uwanja wa Chamazi Complex. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Batenga (kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Steven Mnguto (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NBC yakabidhi Kombe la Ubingwa Championship kwa Kengold FC

**Na Faustine Feliciane**

MABINGWA wa Championship 2024, Kengold FC wamekabidhiwa rasmi kombe la ubingwa na wadhamini wakuu wa mashindano hayo, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Kengold walitwaa ubingwa huo na kukata tiketi ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao pamoja na klabu ya Pamba Fc ya Mwanza waliomaliza katika nafasi ya pili.

Hafla ya kukabidhi kombe hilo ilifanyika jana katika Uwanja wa Chamazi Complex jijini Dar es Salaam ikipambwa na mechi ya kirafiki kati ya mabingwa hao na washindi wa pili (Pamba FC)mechi iliyoisha kwa timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, Elvis Ndunguru, alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi kwenye tukio hilo lililopambwa na uwepo wa Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Batunga likishuhudiwa pia na mamia ya wapenda soka wakiwamo mashabiki waliosafiri kutoka mikoa ya Mbeya na Mwanza. Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Steven Mnguto, alimwakilisha Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia kwenye tukio hilo.

Akizungumza baada ya Kengold kukabidhiwa kombe hilo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Batenga alisema pamoja na kuipongeza timu ya Kengold kwa kuibuka kinara wa ligi hiyo iliyokuwa na ushindani mkubwa miongoni mwa timu shiriki, alishukuru Benki ya NBC kuwa mdhamini mkuu wa ligi hiyo akibainisha kuwa udhamini huo kwa kiasi kikubwa umechochea ushindani kwenye ligi hiyo hatua ambayo anaamini imesaidia kutoa washindi wenye sifa ya kushiriki Ligu Kuu ya NBC msimu ujao.

"Udhamini wa NBC umewezesha kuongeza ushindani kwenye ligi hii na kuboresha soka letu. Leo hii sisi Wanachunya tunajivunia kuwa washindi wa ligi iliyokuwa na ubora kama tulioushuhudia na kupitia ushindani huo tunaamini tunakwenda kutoa changamoto haswa kwenye timu tutakazokutana nazo Ligi Kuu ya NBC. Baada ya ubingwa huu tunakwenda kujipanga kuanzia kikosi hadi benchi la ufundi ili kujiweka sawa zaidi kwa ajili ya Ligi Kuu msimu ujao, tunawakaribisha sana Chunya," alisema Batenga.

Kwa upande wake Ndunguru alisema benki hiyo inayodhamini ligi tatu muhimu hapa nchini, itaendelea kuboresha zaidi ligi hizo ili ziendelee kutoa matokeo chanya kulingana na malengo ya udhamini huo ikiwamo suala zima la kuzalisha ajira ambapo kwa sasa jumla ya ajira 7,000 za moja kwa moja zimezalishwa kupitia udhamini huo.

"Tunawapongeza sana washiriki wote wa Ligi ya Championship lakini kiupekee zaidi tunawapongeza Kengold kwa kuibuka washindi kwenye ligi hii. Pongezi zetu pia tunazielekeza Pamba FC kwa kuwa mshindi wa pili na hivyo anakwenda kushiriki Ligi Kuu ya NBC msimu ujao...hongereni sana," alisema Ndunguru.

## Simba, Azam vita ya nafasi ya pili

INATOKA UK. 24

tatu ambazo ni muhimu sana, leo tutaendelea kumkosa Chama (Clatous) ambaye ni majeruhi na anatumikia adhabu, Miquison, Ntibazonkiza, Onana wote ni majeruhi pia, lakini hiyo sio tatizo kwa kuwa wachezaji waliopo ni waajiriwa wa Simba atakayepewa jezi atatakiwa kutumikia timu na kuhakikisha tunapata ushindi," alisema Mgunda.

Mchezaji wa Simba kwa niaba ya wachezaji wenzake, Hussein Kazi alisema wapo vizuri na wanatambua umuhimu wa mchezo wa leo na kuhakikisha wanapambana kusaka pointi tatu muhimu.

Kwa upande wake, Kocha wa Azam FC, Bruno Ferry alisema mara ya mwisho walikutana na Simba katika mashindano ya Muungano na kupoteza, hivyo wataingia uwanjani kwa tahadhari wakitaka pointi tatu.

Alisema wamejipanga vizuri, wachezaji wapo tayari kwa ajili ya mchezo wa leo na kusaka pointi tatu muhimu mbele ya wapinzani wao kwa ajili ya kufikia malengo yao.

"Ni mechi ya ushindani mkubwa, Simba wako vizuri, tumefanya maandalizi mazuri na wachezaji wapo tayari kwa mchezo, naomba waamuzi kuwa waungwana kwa sababu maamuzi mengi yamekuwa yakiharibiwa, wawe makini ili uwe mchezo wa haki," alisema Bruno.

Nahodha wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda alisema wanataka kulipa kisasi cha kufungwa kwenye mashindano ya Muungano, watapambana kuhakikisha wanapata ushindi.

"Mchezo wa kesho (leo ) ni muhimu kwa kila timu kwa sababu ya kila mmoja wetu anataka pointi kulingana na jinsi alama tulizopishana, tunawafahamu Simba na wao wanatufahamu pia, utakuwa mchezo mgumu, tunapaswa kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu," alisema Lusajo.

## Yanga yaweka dau mezani

INATOKA UK. 24

ni DR Congo yanaendelea," alisema mtoa taarifa hizo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe alibainisha kuwa wapo makini sana katika usajili na wanachokifanya ni kuanza kuangalia na kufanyia kazi mapendekezo ya awali ya benchi la ufundi katika usajili.

"Niwaambie kuwa tutawashangaza watu kwenye usajili ujao, kwa sababu tunahitaji msimu ujao tuendelee kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya ndani na kimataifa, wasubiri kuona kile viongozi wanachofanya," alisema Kamwe.

Michezo
Alhamisi Mei 9, 2024
Nipashe

## Reus apagawa Dortmund kutinga fainali

UKURASA 21



# YANGA YAWEKA DAU MEZANI

●●● Kwa ajili ya kumvuta Kibu Jangwani, Azam nayo...



Kibu Denis

Hersi Said

**Na Saada Akida**

YANGA ni kama imeamua kujiimarisha zaidi kwa ajili ya msimu ujao, inaelezwa chini ya Rais wa klabu hiyo, Hersi Said, wameanza mazungumzo na nyota wa Simba, Kibu Denis.

Mkataba wa mchezaji huyo na Simba unaisha mwishoni mwa msimu huu ingawa Simba wanataka kumbakisha mchezaji huyo, taarifa zinasema tayari uongozi wa Yanga umeingilia kati na kuanza mazungumzo ya kumsajili nyota huyo.

Inaelezwa Yanga wameweka mezani ofa ya shilingi milioni 150 pamoja na gari kwa mchezaji huyo wa zamani wa Mbeya City na tayari uongozi wa Yanga upo kwenye mazungumzo na wawakilishi wa mchezaji huyo.

Imeelezwa kuwa ofa waliyoweka Yanga ni Sh. milioni 150 na gari ikiwa ni sehemu ya ofa yao ya kumuhitaji nyota huyo ambaye mkataba wake unafika ukingoni mwishoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa zilizopatikana jana mchana zinasema viongozi wa Yanga wameanza mazungumzo na nyota huyo na kuweka ofa hiyo mezani lakini Kibu hajatoa tamko lolote la kukubali au kukataa ofa hiyo iliyokwa mezani na mabosi wa Yanga.

Mtoa taarifa amesema Kibu ameingia katika orodha ya wachezaji wanaotakiwa na Yanga baada ya Kocha Miguel Gamondi kutaka kuongezewa mshambuliaji mzawa kwa lengo la kuimarisha safu hiyo ya ushambuliaji.

"Licha ya kuwekewa ofa hiyo hadi sasa Kibu hajasema lolote kuhusu kukubali au kukataa, hii inatokana na kusubiria waajiriwa wake Simba kuhusu ofa yao, pia Azam FC nao wameonyesha nia ya kuhitaji huduma ya nyota huyo," alisema mtoa taarifa hizo.

Alisema Simba nao hawajakata tamaa ya kumbakisha mchezaji huyo kwani nao wamemwekea ofa mezani mchezaji huyo.

"Sasa hivi Kibu ndio mwenye uamuzi kuamua wapi atie saini, ana ofa mbili za uhakika lakini pia Azam wameonyesha nia ya kumtaka pia," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza kuwa mchakato wa usajili unaendelea kwa kasi ndani ya Yanga, baada ya viongozi na benchi la ufundi linaloongozwa Gamondi kukubaliana kuachana na Agustino Okrah na nafasi yake kuchukuliwa na Prince Dube.

"Kuhusu Musonda (Kennedy) kuna uwezekano mkubwa Yanga kubadilishana na mchezaji kutoka TP Mazembe, Phillipe Kinzumbi, mazungumzo kati ya Hersi na Rais wa klabu hiyo ya nchi-

INAENDELEA UK. 23

## Simba, Azam vita ya nafasi ya pili

**Na Saada Akida**

NYASI za Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam leo zitawaka moto katika mchezo wa kusaka heshima na nafasi ya kukata tiketi ya kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Azam FC leo wanakuwa nyumbani kuwakaribisha Simba, kwenye uwanja huo mchezo utakaochezwa saa 12:15 jioni huku timu zote zikihitaji matokeo katika mchezo huo.

Simba wako nafasi ya tatu wakiwa na alama 53 ikiwa na mchezo mmoja mkononi huku wakiwa chini ya Azam kwa tofauti ya pointi nne huku Wanalambalamba hao wakishika nafasi ya pili nyuma ya vinara Yanga.

Katika mchezo wa leo timu zote zinahitaji kupata matokeo chanya na endapo timu yoyote itaibuka na ushindi itajiweka kwenye mazingira mazuri ya kumaliza nafasi ya pili na kuendelea kutoa msukumo kwa Yanga kwenye kuwania ubingwa msimu huu.

Kama Simba ikipoteza mechi ya leo itajiweka kwenye nafasi ngumu ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya kwanza baada ya misimu zaidi ya mitano.

Katika michezo 18 waliyokutana timu hizo, Simba imeshinda mara sita, imepoteza tatu na Azam FC imepata matokeo mara tatu na kupoteza sita, wote wametoka sare mara tisa.

Kuelekea mchezo huo wa leo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda alisema maandalizi ya mchezo wa leo yamekamilika na wapo tayari kushindana kupata matokeo mazuri.

Alisema wanatambua Azam ni timu nzuri yenye kutoa ushindani lakini wamejipanga kufanya vizuri na kuondoka na pointi tatu.

"Siku zote mchezo wa mpira kuna makosa hayakwepeki, kikubwa ni kuyafanyia kazi katika uwanja wa mazoezi, mechi iliyopita tulifanya makosa naamini tumesahihisha na kuyapunguza tayari kwa mchezo wa leo.

„Soka ni mchezo wa wazi hakuna kuficha, tunaingia uwanjani kusaka pointi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >